Nipashe
Jumatatu Juni 13, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580975
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



**UNITED YAJITOSA KUISAKA SAINI YA LEWANDOWSKI**

UKURASA 21

SportPesa
JACKPOT BABA LAO!
TZS. 253,545,950
CHEZA SASA KWA 1000/= TU!
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Msigwa:** Tanzania yaendelea kuandika historia utalii Royal Tour

UKURASA 4



# Padri mwingine auawa kikatili

• **Ni** wa pili raia wa kigeni, uchunguzi wa awali wabaini ni mauaji ya kukusudia... *Endelea Uk.2*



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela (aliyenyoosha mkono), akiteta jambo jana na wajumbe wa kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa huo, walipokwenda Tarafa ya Loliondo, Wilaya ya Ngorongoro, ambako wafugaji wa jamii ya Kimasai wanagomea zoezi la uwekaji wa alama za mipaka katika Pori Tengefu la Loliondo. **PICHA: GODFREY MUSHI**

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**GAVANA BOT, M'BIASHARA LAKE OIL WATWAA TUZO**

GAVANA wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Prof. Florens Luoga na mfanyabiashara wa mafuta, Mkurugenzi Mtendaji wa...

UKURASA WA 4

**POLISI YAMSAKA RAIA WA CHINA MADAI MAUAJI**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linamsaka, Zheng Lingyao (42), raia wa China mkazi wa Dar es salaam

UKURASA WA 5

**HESLB YAZINDUA MFUMO MWAJIRI KULIPA KIMTANDAO**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), imezindua rasmi mfumo wa kidigitali ambao unamwezesha mwajiri...

## Serikali yawasaka wapotoshaji sakata la Loliondo

UKURASA 3



## Mapunye ugonjwa unaotesa watoto

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA YATANGAZA JEURI YA USAJILI UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6



Maambukizi ya ugonjwa wa mapunye yanaweza kutokea hata kwenye sehemu nyingine za mwili kama picha inavyoonyesha. **(PICHA: MTANDAO)**

# Padri auawa kikatili

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

PADRI wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Mbeya wa Shirika la Wamisionari wa Afrika (White Father), Michael Samson (63), amekutwa amefariki dunia katika Mto Meta eneo la Sabasaba jijini hapo, huku mwili ukiwa umekatwa viungo na kutenganishwa.

Mwili wa padri huyo uliokotwa juzi kwenye Mto Meta chini ya Daraja la Sabasaba, ukiwa umeviringishwa kwenye blanketi, huku chanzo cha mauaji hakijajulikana.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Mbeya, Gervas Nyaisonga, Padri Michael alitoweka katika Kituo cha Vijana cha Kanisa Katoliki cha Mbeya Juni 10, majira ya saa 12:00 jioni.

"Padri huyo alikuwa hajulikani alipo mpaka mwili wake ulipokutwa umetupwa Juni 11, mwaka huu saa 4:00 asubuhi maeneo ya Sabasaba jijini hapa 'Raha ya milele umpe ee Bwana' amina," alisema Askofu Nyaisonga.

Taarifa zinasema mwili huo ambao uliviringishwa kwenye blanketi, baadhi ya viungo vilikutwa vimejitenga, kichwa, mkono na mguu vilikuwa umbali kidogo kutoka ulipokuwa umetupwa mwili huo.

Tukio la kifo cha utata cha padri huyo linakuwa ni la pili kutokea ndani ya miezi mitatu, baada ya Aprili 19, mwaka huu Paroko wa Parokia ya Mbezi Mshikamano, jijini Dar es Salaam, Padri Francis Kangwa, kukutwa amefariki ndani ya tangi kubwa la maji lililoko nyuma ya nyumba ya makazi ya mapadri.

Jeshi la Polisi mkoani Mbeya limethibitisha kutokea kwa mauaji hayo, huku likieleza kuendelea na uchunguzi wa kufahamu chanzo cha kifo hicho.

Wakizungumza na vyombo vya habari baadhi ya wananchi wa mkoa huo waliiomba serikali kupitia vyombo vya ulinzi na usalama kufanya uchunguzi ili kuwabaini walioshiriki mauaji hayo na kuwachukulia hatua za kisheria.

Mmoja wa wananchi hao, Gilbert Mhando, dereva bodaboda jirani na eneo hilo, alisema tangu ameanza kufanya shughuli zake katika eneo hilo haijawahi kutokea tukio la kutisha kama hilo, na kuiomba serikali kuchunguza.

Alisema eneo hilo lina taa zinazotumia nishati ya jua na kulifanya muda wote kuwa na mwanga na kuomba ulinzi zaidi.

"Hili tukio limenitisha sana maana hili ndilo eneo ambalo mimi nafanyia shughuli zangu, nilikuwa nimetoka kidogo nimeenda kupeleka abiria sasa ninavyorudi ndiyo nikakuta watu wamekusanyika hapa wanasema kuna mwili umetupwa ndiyo maana nimesogea kuja kuona," alisema Mhando.

Naye Lilian Victor, aliiomba serikali kuweka kamera za usalama katika eneo hilo kutokana na watu kutopita mara kwa mara hasa nyakati za usiku akieleza kuwa endapo pangekuwa na kamera hizo wahusika wangejulikana.

Hata hivyo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi Ulrich Matei, alisema Jeshi hilo linaendelea na uchunguzi wa tukio hilo kubaini chanzo na wahusika wa mauaji hao ili wachukuliwe hatua.

Alisema Jeshi la Polisi linalaani vikali tukio hilo pamoja na matukio mengine ya mauaji ambayo yamekuwa yakitokea katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

"Padri huyo aliwaaga wenzie kwamba alikuwa anakwenda kufanya mazoezi ya kutembea na hakurudi mpaka mwili wake ulipokutwa katika daraja hilo ambalo lipo umbali wa kilomita mbili kutoka eneo wanapoishi," alisema Kamanda Matei.

Kamanda Matei alisema marehemu alikuwa raia wa Malawi na kuwaomba wananchi kutoa taarifa ili kukamatwa kwa wahusika.

Alisema kwa uchunguzi wa awali wamebaini ni mauaji ya makusudi na kwamba Jeshi la Polisi linaendelea kutumia njia za kisayansi ili kumbaini aliyetekeleza mauaji hayo.

Hivyo, aliwataka wananchi kutoa taarifa za siri kwa jeshi hilo kama wanawafahamu wahusika ili watafutwe na wachukuliwe hatua za kisheria.

## Mapunye ugonjwa unaotesa watoto

**Na Jenifer Gilla**

WIMBI la watoto na wanafunzi wa shule za msingi kusumbuliwa na ugonjwa wa mapunye linazidi kushika kasi hali inayowalazimu baadhi ya wazazi kuhusisha ugonjwa huo na imani za kishirikina.

Baadhi ya watoto wanaoshikwa na ugonjwa huo huchukua muda mrefu kupona licha ya kutumia dawa za aina tofauti kuutibu na kujirudia.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wazazi, walisema ugonjwa huo unawapa shida watoto kupona licha ya kuhangaika hospitali mbalimbali kutafuta matibabu.

Rukia Mandia (55), mkazi wa Mwananyamala mwenye mtoto wa kiume anayesumbuliwa na ugonjwa huo kwa zaidi ya miaka sita, alisema mtoto wake alipata ugonjwa huo akiwa na umri wa miaka minne na kuhangaika hospitali mbalimbali bila mafanikio, hali iliyomlazimu kwenda kwa mganga wa kienyeji akiamini mtoto wake karogwa.

"Mwanagu alipata mapunye akiwa na miaka minne, lilianza moja, lakini kadiri siku zinavyokwenda yalikuwa yanaongezeka licha ya kumpeleka hospitali mbalimbali za serikali na binafsi. Mwisho nikaona niende kwa mganga labda mwanangu karogwa si unajua maisha ya uswahilini mtu anaweza kukurogea mwanao bila sababu," alilalamika.

Hata hivyo, alisema haikusaidia na alikata tamaa ya kwenda tena hospitali kutafuta matibabu na kuanza kutumia dawa ya kienyeji, hadi mtoto wake alipofika umri wa miaka 14 ndipo alipopona. Mkazi wa Kiluvya, Janeth Samson, alisema mtoto wake anasumbuliwa na ugonjwa huo kwa muda wa miezi mitatu sasa. Alisema ametumia dawa ya kila aina, lakini bado hajafanikiwa kupata tiba. Prisca Shuma (27), Mkazi wa Manzese, alisema mwanawe anasumbuliwa na fangasi kwa miaka miwili, licha ya kutumia dawa za aina tofauti.

"Alipatwa na hili tatizo akiwa na miaka mitano, punye ni moja tu ila haliishi, nilimpeleka hospitali ya serikali akaandikiwa dawa za vidonge za kutumia siku 21 pamoja ya kupaka, lakini haikusaidia, nimetumia dawa za kienyeji kama vile ndimu, uwatu, unga wa maganda ya maparachichi lakini wapi, hapa sielewi cha kufanya".

Aidan Mushi (45) mkazi wa Tabata, alisema kuwa ingawa mtoto wake alipatiwa matibabu na kupona ugonjwa wa mapunye wanampa elimu ya jinsi ya kujikinga na ugonjwa huo ili usijirudie tena.

### DAKTARI AELEZA

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ngozi kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Magdalena Dennis, alisema mapunye kwa kitaalamu 'Tinea Capitis' ni maradhi ya ngozi yanayosababishwa na fangasi ambao hushambulia zaidi kichwani kwa kuacha mabaka meupe au vipele vyenye maji au usaha.

"Fungus hupenda sehemu zenye mafuta mwilini kama vile usoni, kichwani, sehemu ya juu ya mgongo na kifuani, lakini mazingira ya joto na unyevunyevu yanachochea kuzaliana kwa wingi," alifafanua.

Kwa mujibu wa Dk. Magdalena ugonjwa huo hushambulia watoto zaidi kuliko watu wazima.

### DALILI

Dk. Magdalena alisema baadhi ya dalili za ugonjwa huo ni ngozi kuwasha, mabaka meupe kwenye nywele ambayo yanaweza kuzungukwa na vipele vyenye usaha au vidonda.

### MAAMBUKIZI

Alisema ugonjwa wa mapunye huambukizwa kwa njia nyingi iwapo kuna mazingira rafiki ya kuruhusu fangasi kutoka kwenye kichwa cha mtu mmoja kwenda kwa mwingine ikiwamo hali ya joto pamoja na unyevunyevu.

### KWANINI WATOTO

Watoto wanapata kirahisi maambukizi kwa njia ya kugusana, hasa kutoka kwa aliye na maambukizi kwenda kwa mwingine.

"Kwanza kabisa watoto hawana elimu juu ya mapunye zaidi jinsi ya kujikinga na maambukizi ya maradhi hayo. Kwa hivyo hata akimuona mwenzie ana mapunye hawezi kujizuia asimshike kichwani kwa kuwa hana uelewa wa madhara yake.

"Ndiyo maana ugonjwa huu huwa unawasumbua watoto mpaka atakapofika umri wa kujielewa na kuzingatia usafi," alisema.

Dk. Magdalena alitaja sababu nyingine ni watoto kupata maambukizi kuwa ni kuchangia baadhi ya vifaa vinavyohusisha ngozi kama vile vifaa vya kunyolea bila kuvifanyia usafi wa kuua vimelea kama fangasi.

Sababu nyingine ni kuchangia taulo au nguo ya kujikaushia, kutumia vifaa vya nywele kama chanuo kwa zaidi ya mtu mmoja pamoja na kushirikiana kuvaa mavazi.

Alisema mtu mzima sio rahisi kuambukizwa kwasababu ana tezi inayoitwa kwa lugha ya kitalaamu Sebaceous gland iliyopo kwenye ngozi ambayo husaidia kumharibu na kumuua fangasi huyo.

### MATIBABU

Dk. Magdalena anasema maambukizi hayo hutibika kwa kutumia dawa za kutibu fangasi za kupaka pamoja na vidonge ambavyo mtoto huandikiwa kulingana na uzito wake.

"Hapa niwashauri wazazi wanapoona dalili za mwanzo za watoto wao kuwa na maambukizi ya mapunye wawapeleke hospitali mara moja ili daktari awaangalie na kuwaandikia aina ya dawa kulingana na ukubwa wa tatizo," alisema.

Kwa Mujibu wa Dk. Magdalena mapunye huchukua muda mfupi kuonyesha matokeo mazuri, lakini ni rahisi kwa maradhi hayo kurudi baada ya kumaliza matibabu kama hatua madhubuti za kujikinga na maradhi hayo hazitochukuliwa.

### NINI KIFANYIKE

Dk. Magdalena anasema katika idara yao wanapokea watoto wenye maambukizi hayo wawili hadi watatu kwa siku, pamoja na kuwapa tiba huwashauri wazazi jinsi ya kuzuia usirudi tena. Alishauri wazazi kuhakikisha wanapeleka watoto hospitali na wanamaliza dozi walizoandikiwa ili kuua vimelea vyote vya maradhi hayo.



Mkuu wa Kitivo cha Tiba cha Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU), Prof. Mbembati Naboth, akimkabidhi cheti mmoja wa wanafunzi wa chuo hicho, Khadija Feruz wa mwaka wa pili udaktari ambaye aliwasilisha mada nzuri kwenye mkongamano la kisayansi lililofanyika chuoni hapo, mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Prof. Columba Mbekenga na kulia ni Rais wa Serikali ya Wanafunzi, Nimrodi Matungwa. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Gavana BoT, m'biashara Lake Oil watwaa tuzo

**Na Mwandishi Wetu**

GAVANA wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Prof. Florens Luoga na mfanyabiashara wa mafuta, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Lake Oil, Ally Awadh, wamepata tuzo ya kimataifa ya African Business Leadership Awards (ABLA) 2022.

Waandalizi wa tuzo hizo (ABLA) walisema katika taarifa yao jana kwamba wawili hao waliibuka washindi katika vipengele 13 vya toleo la mwaka huu la ABLA kufuatia upigaji kura uliomalizika Juni 3, mwaka huu.

Chapisho hilo lilisema kuwa tuzo hizo zilishindaniwa na zaidi ya watu 370,000 barani Afrika kupitia kwenye tovuti, mitandao ya kijamii pamoja na mawasilisho kupitia barua pepe na njia ya posta.

Awadh alishinda Tuzo ya Kiongozi Bora wa Biashara kwa Vijana huku Prof. Luoga akishinda Tuzo ya Gavana Bora wa Mwaka wa Benki Kuu.

Lake Oil Group ni moja ya kampuni za Afrika Mashariki zinazokua kwa kasi zaidi katika biashara ya nishati na usafirishaji, ambayo imeongeza wigo wake katika nchi za Zambia, DRC, Burundi, Rwanda, Msumbiji, Uganda, Kenya, Burundi, Sudan, Ethiopia na Canada.

Kwa mujibu wa waandaaji, washindi wa kwanza na wa pili watakabidhiwa tuzo zao katika mkutano wa saba wa Wakuu wa Afrika utakaofanyika Julai 4, mwaka huu nchini Uingereza.

Tuzo hizo ni maalum kutambua kampuni zinazofanya vizuri katika uongozi na biashara barani humo ili kuongeza chachu ya utendaji kazi mzuri.

# Serikali yawasaka wapotoshaji sakata la Loliondo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema imeanza kuchunguza watu waliohusika kutoa taarifa za upotoshaji katika zoezi la uwekaji alama za mipaka ya kutenganisha eneo la makazi na hifadhi la Loliondo na kusababisha vurugu zilizosababisha kifo cha askari mmoja.

Msemaji wa Serikali, Gerson Msigwa, alibainisha hayo jana jijini hapa alipokuwa akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu masuala mbalimbali.

Msigwa alisema vyombo vya dola vipo katika uchunguzi wa kubaini wahusika wote waliotoa taarifa za upotoshaji ambazo zilisababisha wananchi kuwavamia wataalam wa serikali ambao walikuwa wakiweka mipaka katika eneo hilo.

"Vyombo vya dola hivi sasa vinafanya uchunguzi ili kubaini watu ambao wamehusika katika kutoa taarifa za upotoshaji zilizosababisha vurugu zile na hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

"Hatua kali zitachukuliwa bila kujali cheo cha mtu kwasababu nchi yetu inaongozwa kwa mujibu wa sheria na hatukatazi mtu kutoa taarifa, lakini kupotosha au kufanya uchochezi ni kosa hatuwezi kumvumilia mtu wa aina hiyo," alisisitiza Msigwa.

Alisema kitu ambacho Watanzania wanapaswa kufahamu hakuna askari ambaye serikali imemtuma kwenye eneo hilo kuwatoa wananchi, bali kilichokuwa kinafanyika ni kuweka mipaka kati ya eneo la makazi na hifadhi.

Alisema jambo hilo la kuweka mipaka sio geni na wala sio mara ya kwanza kwa serikali kufanya hivyo, tayari imefanya hivyo katika maeneo mengine kwa nia njema.

**ACT-WATAKA TUME HURU**

Wakati huohuo, Chama cha ACT-Wazalendo, kimeitaka serikali kuunda tume huru kwa ajili ya kuchunguza tukio la vurugu zilizotokea Juni 10, mwaka huu, katika Tarafa ya Loliondo na Sale, Wilaya ya Ngorongoro, Mkoa wa Arusha

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Waziri Mkuu kivuli wa chama hicho, Dorothy Semu, ni muhimu tume hiyo kuwa na uwakilishi wa jamii ya kimasai ili ifanye uchunguzi wa kilichotokea siku hiyo.

Alisema tume hiyo itaweza kuainisha ukweli kuhusu vifo vya raia, polisi na majeruhi, pamoja na sintofahamu ya uhusika wa wafugaji wa nchi jirani ya Kenya na uvunjifu wa haki za binadamu katika eneo hilo.

Semu alisema ni wakati wa serikali kutumia njia ya majadiliano na ushirikishwaji ili kutafuta suluhu ya matatizo katika eneo hilo ikiwa ni pamoja na kukaa na wafugaji na wananchi wanaoishi katika vijiji hivyo kutafuta suluhu.

Aidha, alisema ni wakati mwafaka kwa Rais Samia Suluhu Hassan, kusitisha azma ya kupandisha ardhi ya vijiji kuwa pori la akiba ili kulinda haki za wenyeji ambao ni ardhi yao.

"Hili la kusitisha lisiwe kwa Loliondo tu bali kwa nchi nzima, kwani kwa mujibu wa Sheria namba 5 ya Uhifadhi wa wanyama pori ya mwaka 2009 Waziri wa Maliasili na Utalii anatakiwa aondoe mapori tengefu vijijini," alisema.

Semu alisema kitendo cha kushindwa kuwashirikisha wafugaji wa jamii ya Kimaasai katika suala zima la Loliondo na Ngorongoro kwenye kutatua matatizo yao inainyima serikali kupata mawazo mbadala.

Alisema serikali inafahamu kuwa Juni 22, mwaka huu, Mahakama ya Afrika Mashariki, itatoa hukumu ya kesi iliyofunguliwa na vijiji vinne mwaka 2017, ikiwa ni jitihada za wananchi wa Loliondo na Sale kutafuta mwafaka kwa kujadiliana na viongozi wa serikali.

Aliongeza kuwa vijiji hivyo pia vilifungua shauri namba 15 la mwaka 2017 kuiomba mahakama kuizuia serikali kuacha kufanya jambo lolote katika eneo hilo, hadi kesi ya msingi itakapoamuliwa, Septemba 25, 2018 mahakama iliamuru serikali kusubiri hukumu ya kesi ya msingi.

**ANATAFUTWA**



Ndugu **Mariam Hussein Lindwe** pichani anatafutwa na polisi Kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo vya kinyume na maadili na Wizi wa kuaminiwa, Taarifa imeripotiwa polisi **No. BUG/RB/1245/2022, Tarehe 12/4/2022** yeyote mwenye taarifa zake anaombwa atoe taarifa polisi kituo cha karibu nae.

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya SENGEREMA**
**Kituo cha NYAHUNGE Mkoa MWANZA**

**Shauri la Madai/ Ndoa Na 19 /2022 na SHAURI NO. 18/2022**
**Jina la Mdai ISAKA MASHAURI KIRASA**
**Jina la mdaiwa 1. REBEKA JOSEPH- 0752 510037**
**2. NYADHI INVESTMENT CO. LTM AUCTION MART**
**(DALALI WA MAHAKAMA) (0768588155)**

**KUITWA SHAURINI**
(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika mahakama za mwanzo)

**Kwa REBEKA JOSEPH WA KISEKE "A" ILEMELA MWANZA.**
Kwa kuwa mdai/ wadai ameleta /wameleta madai yake/ yao kwamba .kuja kujibu pingamizi la utekelezaji lililo wasilishwa hapa na Isaka Mashauri Kirasa na Christina Lugata hiyo unatakiwa kuudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 17 mwezi 06 mwaka 2022 saa 08:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/ mashaidi wako na vielelezo vyote vinavyo husu shauri hili kwajili ya kujitetea
**ANGALIZO:** Kama hutohudhuria siku iliyo tajwa hapo juu na kuthibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 08 mwezi 06 mwaka 2022

............
**HAKIMU**

Total Fiscal Solutions

**KUSITISHA AJIRA YA BW. OPHORO DOMINICK LYATUU.**



Kampuni ya **TOTAL FISCAL SOLUTIONS LIMITED** Tawi la Mwanza inapenda kuufahamisha umma ya kwamba Bw. **OPHORO DOMINICK LYATUU,** aliyekuwa ameajiriwa kama Afisa Mauzo **SIO MFANYAKAZI** wa Kampuni hii kuanzia tarehe 30-05-2022 na hivyo Kampuni haitahusika na chochote atakachofanya kwa niaba ya Kampuni ya **TOTAL FISCAL SOLUTIONS LIMITED.**

216896702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Baruapepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa kampuni ya **PMM ESTATES (2001) LTD** itasafirisha mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **IKUNGI-SINGIDA** kwa gari zenye namba za usajili **T600DVW/T166DUL,T590DVW/T170UL,T573DVW/T103DUL,T584DVW/T158DUL.** Safari imepangwa kuanza tarehe **12.06.2022**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 17.5**
   **Upana - mita 4.2**
   **Kimo - mita 4.8.**
3. Njia itakayotumika ni **DAR ES SALAAM** hadi **SINGIDA** kupitia **PWANI, MOROGORO, DODOMA.** Gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza*

216898402

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**AT DODOMA**
**MATRIMONIAL NO.7 OF 2020**
**MILEMBE BUNDALA .............................**
**APPELLANT/APPL/PLAINTIFF**
**VERIUS**
**MKUBA SHIBE..................RESPONDENT**
**DEFENDANT**
**TO.........MKUBA SHIBE**

**NOTICE OF DATE OF HEARING**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for/hearing/mention on 11 day of 07 2022 at 9:00 am. Before **Hon. A. MAMBI.............. JUDGE**
**YOUR ARE** required to appear in this Court on the fixed date without fail. And you may bring with you all required documents in support of your case.
**Given under my hand and the seal of the Court this 08 day of 06,2022.**

**NAFASI ZA KAZI**

1. **Wakaguzi wa Shule:** Sifa awe mwalimu mstaafu
2. **Mhasibu Diploma au Cheti** Sifa awe msichana umri kati ya miaka 20-25

Maeneo ya kazi ni mbande karibu na Azam, pia waombaji wawe wanaojua kutumia computer

**MAWASILIANO 0753 382833**




Balozi wa Uholanzi nchini Tanzania, Wiebe de Boer, akizungumza na wadau wa masuala ya uwekezaji kutoka Uholanzi na Serikali ya Tanzania katika mdahalo uliojadili vikwazo, changamoto za kibiashara na fursa za uwekezaji baina ya nchi hizi mbili, uliofanyika jijini Arusha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Msigwa: Tanzania yaendelea kuandika historia utalii

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TANZANIA imeendelea kuandika historia katika maendeleo ya sekta ya utalii baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kurekodi filamu ya Royal Tour iliyozinduliwa hivi karibu. Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, Msemaji Mkuu wa Serikali Gerson Msigwa, alisema matokeo ya kazi kubwa iliyofanywa na Rais Samia, yameanza kuonekana kutokana na idadi ya watalii kuanza kuongezeka kwa kasi kubwa katika maeneo ya vivutio vya utalii na hoteli.

"Takwimu kutoka Hifadhi za Taifa (TANAPA) zinaonyesha Aprili na Mei 2022 idadi ya watalii waliotembelea maeneo yetu ya hifadhi 22 yanayojumuisha Serengeti, Manyara, Mikumi, Nyerere, Udzungwa, Ruaha imeongezeka hadi kufikia watalii 115,198 ambapo kati yao watalii wa ndani 71,593 na watalii wa nje 43,605 ikilinganishwa na watalii 59,664 ambapo watalii wa ndani 46,624 na watalii wa nje 13,040 wa Aprili na Mei mwaka jana," alisema.

"Ongezeko hili pia limeongeza mapato kutoka Sh. bilioni 5.7 hadi kufikia Sh. bilioni 15.559.

Aidha, alisema katika Hifadhi ya Eneo Maalum la Ngorongoro, takwimu zinaonyesha kuwa katika kipindi cha Aprili na Mei 2022, idadi ya watalii imeongeza hadi kufikia 51,044, wa ndani ni 25,150 na wa nje 25,894 ikilinganishwa na 22,954 wa Aprili na Mei mwaka 2021. Alisema mapato kutoka Ngorongoro kwa kipindi hicho yameongezeka kutoka Sh. bilioni 2.585 hadi kufikia Sh. bilioni 10, likiwa ni ongezeko la asilimia 289.

"Tumeanza kupokea ndege za moja kwa moja kutoka nchi mbalimbali na juzi tu mmeona kampuni ya EUROWING ambayo ni mwanachama wa Lufthansa Group, imeanza safari za moja kwa moja kutoka Frankfurt, Ujerumani hadi Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), ndege hii itakayokuwa inakuja moja kwa moja ina uwezo wa kubeba abiria 302 na itakuwa ikifanya safari mbili kwa wiki," alisema Msigwa.

Alisema pia, kampuni nyingi za ndege ambazo zilikuwa zimesitisha safari zake nchini zimeanza kurudi hali ambayo inaweza kuongeza watalii zaidi nchini.

"Kampuni nyingi za ndege ikiwamo ya Uturuki ambayo ilisitisha safari zake sasa itaanza safari mara nne kwa wiki la itatumia ndege aina ya Airbus ambazo zinabeba abiria zaidi ya 300, hivyo tunaweza kuwa na watalii wengi kwa wiki wanaokuja kutembelea vivutio vyetu nchini.

Kadhalika, alisema lengo la serikali ni kufikisha watalii milioni tano kwa mwaka ifikapo 2025.

Msigwa aliwataka Watanzania kushiriki zoezi la sensa linalotarajia kufanyika Agosti 23, mwaka huu nchini.

Alisema ni muhimu kila mtu kushiriki sensa ili kuiwezesha serikali kupata takwimu sahihi zitakazo tumika kupanga bajeti zake.

"Sensa ya mwaka huu ni ya kidijitali zaidi lazima kila mmoja wetu ashiriki ili tuwe na sensa bora ambayo mataifa mengine yatakuja kujifunza," alisema.

Alisema maandalizi ya sensa yamefikia asilimia 88 na ugawaji wa maeneo ya kuhasabia watu kwa Zanzibar na Tanzania Bara yamefikia asilimia 100 kinachoendelea hivi sasa ni utoaji wa elimu kwa wananchi. "Pia katika zoezi la uwekaji wa anwani za makazi limefikia asilimia 95 kwa makazi zaidi ya milinio 12.3 tayari yameshawekewa anuani, natoa wito kwa watu wote ambao bado kwenda kwa viongozi wao wa mitaa ili waweze kupata anwani hizo," alisema Msigwa.

# Polisi wamsaka raia wa China tuhuma mauaji

**Na Jenifer Gilla**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linamsaka, Zheng Lingyao (42), raia wa China mkazi wa Dar es Salaam kwa tuhuma za kumuua, Fu Nannan, (26), ambaye ni raia wa China.

Akizungumza na Nipashe, Kamanda wa Polisi wa kanda hiyo, Jumanne Muliro, aliithibitishia Nipashe kuwa bado mtuhumiwa huyo hajapatikana na juhudi za kumtafuta zinaendelea.

"Ni kweli tunamtafuta mpaka sasa bado hatujamkamata na juhudi zinaendelea kuhakikisha kuwa tunamkamata ili afikishwe kwenye vyombo vya sheria," alisema.

Akizungumza undani wa tukio hilo, Kamanda Murilo alisema mtuhumiwa huyo alifika eneo la Ilala na marehemu alikuwa anaishi kwenye ghorofa ya tatu ya wapangaji na kumjeruhi kwa risasi tumboni, Nie Mnqin, kisha kumfyatulia risasi Nannan ambaye baadaye alifariki dunia.

Kwa mujibu wa Kamanda Muliro, tukio hilo limetokea Juni 11, 2022 majira ya usiku katika Mtaa wa Kalenga, Ilala kwenye nyumba ya marehemu aliyokuwa anaishi.

Kamanda Muliro alisema kwa sasa Mnqin anaendelea na matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), uchunguzi wa awali umebaini chanzo ni kutoelewana katika suala la mapenzi.

# Askari aliyeuawa kwa mshale kuzikwa leo

**Na Thobias Mwanakatwe,** ARUSHA

MWILI wa askari aliyeuawa kwa kuchomwa mshale katika Tarafa ya Loliondo, Wilaya ya Ngorongoro mkoani Arusha, Garlus Mwita, unatarajia kuzikwa leo katika Kata ya Kiagata, Wilaya ya Butiama, mkoani Mara.

Askari huyo mwenye namba G4200, ambaye alikuwa na cheo cha koplo, alifariki mwishoni mwa wiki baada ya kuchomwa mshale wakati wa uwekaji alama za mipaka katika eneo la pori tengefu la Loliondo.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Raymond Mangwala, alisema mwili wa askari huyo ambaye alikuwa akifanya kazi Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Dodoma, umeagwa jana katika ibada iliyofanyika viwanja vya ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro.

"Unavyoongea na mimi ni kwamba tupo katika ibada ya kuaga mwili wa marehemu na baada ya zoezi la kuaga kukamilika utasafirishwa kwa ndege hadi wilayani Butiama mkoani Mara ambako atazikwa leo (Jumatatu)," alisema.

Mangwala alisema ibada ya kuaga mwili huo ilihudhuriwa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, Kamishna wa Opereshni na Mafunzo, Liberatus Sabas, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo.

Aliwataka wengine ni viongozi kutoka kamati za ulinzi za Mkoa wa Arusha na ya Wilaya ya Ngorongoro, viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na wananchi.

Wakati huohuo, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mongella jana, alishiriki zoezi la uwekaji wa alama za mipaka katika pori tengefu la Loliondo eneo la Ndorobo wilayani Ngorongoro.

HABARI KITAIFA

# HESLB yazindua mfumo mwajiri kulipa kimtandao

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), imezindua rasmi mfumo wa kidigitali ambao unamwezesha mwajiri kuwasilisha makato na orodha ya wanufaika (wafanyakazi) wake kwa njia ya mtandao kutoka popote alipo.

Akizindua mfumo huo jana, jijini hapo, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, alisema ulianza kwa majaribio mwaka 2019/20 na sasa umekamilika na kuwawezesha waajiri na wanufaika kurejesha mkopo kwa urahisi.

"Zamani ilikuwa mwajiri inabidi atoke ofisini kwake aje HESLB kufanya malipo, lakini kwa sasa anaweza kuwasilisha orodha ya wanufaika-wafanyakazi wake na makato kutoka popote alipo kwa kutumia mfumo wetu huu ambao anajiunga kupitia tovuti yetu (www.heslb.go.tz)," alisema Mkurugenzi Mtendaji huyo.

Mfumo huo pia unamwezesha mnufaika mmoja mmoja kupata taarifa za deni lake na utaratibu wa kurejesha kupitia tovuti ya HESLB.

"Kuanzia mwaka jana, imekuwa ni rahisi sana, unaingia kwenye tovuti

yetu, unabofya 'rejesha mkopo' au 'repay loan' na kufuata maelekezo ya kujisajili na utaendelea kupata taarifa ya deni lako palepale au hata kudai refund (makato yaliyozidi)," alisema Badru.

Akizungumzia uzoefu wake katika kutumia mfumo huo, Mwakilishi wa Shule ya Msingi Young Jai, jijini hapo, Young Mi Cha alishauri HESLB iboreshe mfumo huo ili kuwawezesha waajiri kuwatambua waajiriwa wapya kama walinufaika na mikopo ya elimu ya juu.

"Kuna wakati waajiriwa wapya wanadanganya hivyo pamoja na uzuri wa mfumo huu, ninashauri uboreshwe ili mwajiri aweze kutambua mwajiriwa mpya kama ni mnufaika wa HESLB au hapana bila kumuuliza au kuleta jina kwenu kwa uhakiki kwanza," alisema Young.



Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Eliamani Sedoyeka (kushoto), akizungumza na Ujumbe wa Benki ya NMB, ulioongozwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna (kulia), walipomtembelea ofisini kwake jijini Dodoma. Wapili kulia ni Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa benki hiyo, Filbert Mponzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Uhaba matundu ya vyoo wachangia watoto kufanyiana ukatili kijinsia'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

UHABA wa matundu ya vyoo kwenye shule mbalimbali nchini, umetajwa kuwa chanzo cha vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwamo unajisi kwa wanafunzi.

Mwenyekiti wa Sauti ya Jamii Kipunguni, mkoani Dar es Saalam, Fatma Talib, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza kwenye mkutano wa mashauriano kati ya wabunge wanawake na wabunge vinara wa jinsia kuhusu masuala ya kibajeti.

Mkutano huo ulilenga kuishauri serikali kuwa na bajeti yenye mlengo wa kijinsia ili kujibu kero mbalimbali zinazowakabili wanawake na watoto nchini.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Talib alisema katika Wilaya ya Ilala anakotoka, kero ya matundu ya vyoo kwenye shule za msingi imekuwa ikisababisha wanafunzi kunajisiana wao kwa wao.

"Unakuta tundu moja la choo linatumiwa na watoto hata 200 hivyo ule msongamano unasababisha vitendo vya kunajisiana kwa watoto katika shule zetu."

"Kuna shule moja kule kwangu matukio ya kunajisiana kwa watoto na kufanyiana vitendo visivyokuwa vya kimaadili yalitokea na hii yote ilikuwa ni kutokana na uhaba wa matundu ya vyoo hivyo kusababisha msongamano wa watoto katika maeneo ya vyooni," alisema.

Pia, uhaba huo umekuwa kero kwa wasichana hasa wanapokuwa katika kipindi chao cha hedhi kwa kukosa eneo la kwenda kujisitiri. Alisema serikali inapaswa kuanza kutenga bajeti yenye mlengo wa kijinsia ambayo itasaidia shule nyingi kuwa na vyumba kwa ajili ya mabinti kujisitiri.

"Tunashukuru kwa fedha za UVIKO-19 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, lakini sasa ipo haja ya kuanza kujenga vyumba kwa ajili ya mabinti zetu kujisitiri, lakini pia huduma ya maji ni muhimu sana katika shule zetu hivi sasa watoto wanakwenda na vidumu vya maji shuleni," alisema.

Naye, Kwangu Limbu, kutoka Kishapu mkoani Shinyanga, alisema katika kijiji cha Kiloleli anakotoka wanakabiliwa na kero kubwa ya ukosefu wa huduma ya maji hali inayosababisha watoto wengi kuacha shule.

"Tunaomba serikali ituangalie wakati inapopanga bajeti yake sisi maji tunayapa umbali zaidi ya kilomita 15 na siyo safi na salama kwa matumizi ya binadamu, lakini kwakua tunafuata mbali tunalazimika kutoka majumbani saa mbili usiku na kurudi asubuhi hali hii inasababisha watoto kuacha shule za sisi ndoa zetu kuvunjika," alisema.

Kwa upande wake, Mwezeshaji kutoka Mtandao wa Kijinsia Tanzania (TGNP), Deogratius Temba, aliishauri serikali kuongeza ruzuku ya kila mwanafunzi kutoka Sh. 10,000 ya sasa hadi Sh. 25,000.

Alisema kiasi hicho kitasaidia shule kujiendesha na kuwezesha huduma mbalimbali kwa wanafunzi ikiwa ni pamoja na kuwapatia taulo za kike wanafunzi wa kike.

"Kiasi cha Sh. 10,000 ni kidogo sana kimekuwa kikitumika kwa zaidi ya miaka 20 sasa, hivyo ni wakati mwafaka sasa kuongeza hadi Sh. 25,000 ili kukidhi hali ya mabadiliko ya uchumi kwa sasa na kusaidia kutoa huduma kwa wanafunzi za uji pamoja na taulo za kike ili watoto washiriki masomo bila kukosa," alisisitiza Temba.

Vilevile, aliishauri serikali kuandaa mwongozo wa bajeti ambao utazilazimisha Halmshauri zote nchini kuwa na bajeti zenye mlengo wa kijinsia ili kutoa taulo za kike kwa wanafunzi pamaoja kuandaa vyumba vya kujistiri wanapokuwa hedhi.

Mwenyekiti wa chama cha Wabunge wanawake Magreth Sitta, alisema mambo yaliyoshauriwa na wadau hao wabunge wataishauri serikali ili yafanyiwe kazi.

# Watumishi h'shauri Kondoa matatani tuhuma kuzidisha malipo mradi maji

**Na Renatha Msungu,** KONDOA

WATUMISHI watatu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, wameburuzwa mahakamani kwa tuhuma za kuzidisha malipo kwenye Mradi wa Maji Mlongia, wilayani humo na kuisababishia serikali hasara ya Sh. milioni 117.8.

Washtakiwa walifikishwa mahakamani mwishoni mwa wiki mbele ya Hakimu wa wilaya hiyo, Mwajuma Lukindo, wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi.

Akitoa maelezo mbele ya Hakimu huyo, Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), Leonard Haule, alidai washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka sita ikiwamo matumizi ya nyaraka na kumdanganya mwajiri na kuisababishia serikali hasara hiyo kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Pia, alidai shtaka la sita linalowakabili ni kutumia hati tofauti za malipo ya kazi ambazo hutumiwa na serikali kutoa malipo.

Aliwataja washtakiwa kuwa ni Mhandisi mstaafu wa Wilaya ya Kondoa, Ally Mruma, Mafundi Sanifu wa Maji, Merinyo Saning'o na Hussein Modu.

Alisema washtakiwa walitenda kosa hilo mwaka 2018 kwenye mradi huo baada ya kuzidisha malipo kwenye hati namba moja, mbili na tatu ya madai halisia ya kazi waliokabidhiwa kuifanya.

Washtakiwa hao walikana mashtaka hayo na kuachiwa kwa dhamana, kesi hiyo imepangwa kuanza kusikiliza hoja za awali Juni 29, mwaka huu.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA U J E N Z I , UCHUKUZI NA**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
21.03.2022

# TANGAZO

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **14.06.2022** hadi **27.06.2022** kampuni ya **Spedag Interfreight** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Holili kuelekea Moshi**, gari hilo lenye namba za usajili:

**KCJ943F/ZE1097, KCM104W/ZF0174**
**KBQ622Z/ZE0978, KCK293W/ZE2585**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo
**Urefu - Mita 21** **Upana - Mita 4.15** **Kimo - Mita 5.15**

3. Njia itakayotumika: **Holili** hadi **Moshi** kupitia **Soweto**, gari litasafiri muda wa mchana tu (**Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni**)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga sajilini kwa malengo na si kushindana

LICHA ya kwamba Ligi Kuu Tanzania Bara haijafikia ukingoni ili kutoa nafasi ya dirisha kubwa la usajili kufunguliwa, tayari tetesi za usajili zimeanza kupamba moto kwa miamba ya soka nchini Simba na Yanga.

Ikumbukwe miamba hiyo tayari ina tiketi mkononi ya kuipeperusha bendera ya Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa msimu ujao, michuano ambayo huandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika, CAF.

Yanga ambayo inaongoza Ligi Kuu ikiwa na pointi 64 inafuatiwa na Simba yenye alama 51, pointi hizo zikiwa haziwezi kufikiwa na timu yoyote kwenye msimamo ligi hiyo msimu huu, hivyo timu hizo zina uhakika wa kumaliza katika nafasi ya kwanza na ya pili.

Hivyo, kwa kuzingatia ukweli kwamba msimu ujao Tanzania itawakilishwa na timu nne; mbili zitakazomaliza nafasi ya kwanza na ya pili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho Afrika, kwa itakayoshika nafasi ya tatu kwenye Ligi Kuu kupata nafasi hiyo huku mshindi wa nne ikitegemea na endapo bingwa wa Ligi Kuu ndiye atatwaa Kombe la FA.

Kwa mujibu wa kanuni za Shirikisho la Soka nchini (TFF), mshindi wa Kombe la FA huiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, hivyo kutokana na msimu huu Yanga ambayo ina nafasi kubwa ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu, kutinga fainali ya FA Cup ikitarajiwa kucheza dhidi ya Coastal Union, endapo Coastal haitabeba taji hilo, basi timu itakayomaliza nafasi ya nne itaiwakilisha nchi kwenye michuano hiyo ya CAF.

Hivyo, kutokana na wakongwe hao wa soka nchini, Simba na Yanga kuwa na uhakika wa kushiriki Ligi ya Mabingwa, zimekuwa zikihusishwa na wachezaji wengi huku jina la nyota wa Asec Mimosas ya Ivory Coast raia wa Burkina Faso, Stephane Aziz Ki, likizidi kugonganisha vichwa vya habari kwa klabu hizo kubwa nchini.

Presha imekuwa kubwa kuanzia kwa mashabiki hadi viongozi wa klabu hiyo, kila mmoja akitaka kuona wanafanya usajili mkubwa wakuvutia kuelekea msimu ujao ambao miamba hiyo inaeleza kupania kufanya vizuri kimataifa.

Kutokana na presha hiyo, Nipashe tunaona kunauwezekano ikawapoteza viongozi wa klabu na wote waliopewa jukumu la kufanya usajili, wakajikuta wakisajili kwa ushindani wa nani zaidi badala ya kufuata maoni na mapendekezo ya mabenchi yao ya ufundi ili mwisho wa siku waweze kutimiza malengo waliowekewa.

Tumelazimika kukumbusha hilo hasa kutokana na uzoefu mkubwa tulionao katika kipindi cha usajili hususan kwa klabu hizo mbili, ambazo huishia kushindana katika mbio za usajili na mwisho wa siku kujikutana zikisajili wachezaji wengi wa nafasi moja na kusahau mapendekezo muhimu kutoka kwa makocha wao.

Ikumbukwe pia nafasi za kusajili wachezaji kutoka nje ya nchi ni 12 tu, ambazo ni chache sana, hivyo viongozi wa Simba na Yanga hawana budi kuwa makini kwa kusajili wachezaji katika nafasi muhimu ambao wanaona ni nadra kupata wazawa wakukidhi viwango wanavyohitaji.

Tunataka kuona wachezaji wanaosajili kutoka nje wanakuja kutoa mchango mkubwa kwa klabu hizo na si kusajili wakuja kukaa benchi kutokana na kuzidiwa ama kuwa na ubora sawa na wazawa.


Hivyo, hiki si kipindi cha Simba na Yanga kuanza kukimbizana katika kuonyeshana jeuri ya fedha kuelekea dirisha la usajili, badala yake tunataka kuona kila klabu ikisajili kutokana na mapendekezo ya mabenchi yao ya ufundi ikiwa ni pamoja na wachezaji waliowafuatilia kwa muda mrefu.

Aidha, viongozi wa klabu hizo hawana budi kutumia vema nafasi hizo 12 kwa umakini mkubwa kwa kusajili wachezaji wenye viwango vya juu huku wakimulika kwa umakini historia yao ya majeraha ili kuepuka wale wakucheza mechi moja inayofuata wanakuwa nje ya uwanja wakijiuguza kwa kipindi kirefu.

Tunaamini kama klabu hizo kongwe nchini, zitaacha mashindano katika mbio za usajili na kufuata kile ambacho mabenchi yao ya ufundi yamependekeza, zinaweza kupata wachezaji wazuri watakaowasaidia kwenye michuano ijayo ya kimataifa na kufika mbali.

Lakini lengo letu ni kuona usajili unaofanywa unakuwa wa tija na kuzaa matunda kwa angalau msimu huu tushuhudie timu zaidi ya moja zikitinga hatua ya robo fainali, nusu na hatimaye fainali kwenye michuano hiyo ya CAF, na hilo litawezekana tu kama zitatuliza kichwa kuelekea kipindi hiki cha usajili na si kusajili kwa mashindano.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ligi Kuu msimu ujao ianze mapema kuisuka Stars

Na Adam Fungamwango

**BAADA** ya kipigo cha nyumbani cha mabao 2-0 dhidi ya Algeria kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, baadhi ya mashabiki wa soka nchini ni kama vile wameanza kukata tamaa na timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars.

Wanaona kama hadithi inaweza kuwa ni ile ile ya kushindwa kufuzu kucheza fainali za Mataifa ya Afrika, AFCON kwa mara nyingine tena.

Kinachowanyong'onyeza ni kuona ni kama hadithi inajirudia tena. Ya kutoka sare ugenini na kufungwa nyumbani. Wanakumbuka wakati ule Stars ilipokuwa ikisaka tiketi ya kwenda kucheza fainali za Kombe la Dunia linalotarajiwa kufanyika baadaye mwaka huu nchini Qatar.

Ni kwamba ilikuwa inatoka sare na kushinda ugenini, huku ikipoteza nyumbani. Ilitoka sare ugenini dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na kuifunga Benin nyumbani kwao, lakini tatizo ilikuwa haifanyi vizuri nyumbani, ndiyo maana ilifungwa na timu hizo mbili hapa nchini kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Naona mashabiki wengi wameanza kukumbuka hilo baada ya mechi ya kwanza kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Niger, kabla ya kuchapwa dhidi ya Algeria.

Kwa sasa Tanzania ipo chini ya Algeria na Niger, ikiwa na pointi moja, sawa na Uganda kwenye Kundi F. Ni timu mbili tu zinatakiwa kufuzu kwenda kwenye fainali hizo zitakazochezwa mwakani nchini Ivory Coast.

Pamoja na yote haya, Stars bado haijapoteza na inaweza kufanya vema kwenye mechi zilizosalia ikakaa nafasi ya kwanza au ya pili.

Kikubwa ni maandalizi, pamoja na wachezaji kulinda viwango vyao. Ukisikiliza mashabiki wanavyolaumu, wanaongeza vitu vya juu juu tu ambavyo ni matokeo ya vitu vya msingi. Wengine wanalaumu kocha hasa kwenye upangaji, wengine wanalaumu baadhi tu ya wachezaji.

Ukweli tu ni kwamba ule ndiyo uwezo halisi wa wachezaji wa Tanzania ulipofikia. Na ukiangalia bado hawakucheza vibaya sana, ila kwenye mechi dhidi ya Algeria walikutana na timu yenye wachezaji wakubwa, wanaocheza timu kubwa barani Ulaya, ambao walicheza kikubwa.

Wakati Stars ikikosa mabao, wenyewe walizitumia nafasi chache tu walizozipata kupata mabao. Kuna walidai kuwa yote inatokana na nchi yetu kuwa na wachezaji wa kigeni kwenye ligi yetu, hivyo linapokuja suala la timu ya taifa tunajikuta hatuna wachezaji bora. Wale ambao tunawaona na kuwaimba kuwa ni bora kwenye ligi yetu ndiyo tunashtuka kuwa si Watanzania.

Hapa ndipo kuna mshangao kidogo, kwani wachezaji karibuni wote wa Algeria hawakutoka kwenye ligi ya nchi hiyo. Wengi wanacheza klabu kubwa barani Ulaya.

Ina maana siyo lazima uwe na wachezaji wa timu ya taifa wanaotoka kwenye ligi ya nyumbani. Unaweza wote ukawatoa nje ya nchi. Ndiyo timu za taifa za wenzetu wamefikia huko. Nilitegemea mashabiki wangewashauri wachezaji wa Kitanzania nao sasa wengi wao watoke nje ya nchi ili ikiitwa Stars, basi wachezaji wa ndani wawe wawili watatu wakujazia tu kama wanavyofanya wenzetu.

Pamoja na yote haya, mechi zijazo zitachezwa Septemba. Stars itakuwa ugenini Septemba 19 dhidi ya Uganda. Huu ni muda mrefu wa kujipanga kuanzia wachezaji wenyewe na Shirikisho la Soka nchini (TFF), kama kweli tuna nia ya kufuzu.

Kwa upande wa wachezaji wanatakiwa kujitunza na kujituma kwenye klabu zao. Itashangaza kuona mwezi huo unafika, nusu nzima au robo tatu ya wachezaji hawapo kwa sababu hawakuitwa kutokana na viwango vyao kushuka. Hili ndilo tatizo kubwa la wachezaji wetu. Stars inachaguliwa kwa viwango vya wakati huo na si vinginevyo.

Kwa upande wa TFF ni wakati wa kuangalia kuiwahisha Ligi Kuu msimu ujao ili ikifika Septemba 19 angalau wachezaji wawe kwenye fomu.

Ligi msimu huu imechelewa kumalizika, huku fainali ya Kombe la FA ikichezwa Julai 2, sasa kama mwezi Agosti utapita hivi hivi na ligi ikaanza mwanzoni au katikati ya Septemba, itakuwa ngumu sana kushinda mechi zinazofuata na kufuzu.

Wachezaji watakuwa bado hawako fiti, kwani wengi watakuwa wanajitafuta kwa sababu ya kutoka kwenye mapumziko marefu. Hata kocha jinsi ya kuchagua itakuwa shida.

Nashauri tu angalau ligi ianze katikati ya mwezi Agosti, ili mpaka mechi ya Uganda inafika, tayari wachezaji wameshaanza kuchangamka, na hata unaweza kuwapata wachezaji wapya ambao wameonyesha viwango bora.



Mstaafu akikabidhiwa cheti na zawadi ya shilingi milioni mbili na mgeni rasmi Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Wizara ya Maliasili na Utalii, Prisca Lwangili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtoto afariki dunia kunywa sumu ya magugu

**Na Said Hamdani, LINDI**

MTOTO wa miaka mitatu, Feisari Mponda, mkazi wa Kijiji cha Sinde, Kata ya Madangwa, Mkoa wa Lindi, amefariki dunia baada ya kunywa sumu ya kuua magugu shambani.

Akizungumza na Nipashe, shangazi wa mtoto huyo, Sikudhani Khalfani, alisema Feisari alifariki dunia juzi katika Hospitali ya Mkoa ya Sokoine.

"Hii sumu iliwekwa kwenye chupa za majisafi, huyu mtoto alipoiona aliichukua na kuinywa akifikiri ni juisi," alisema.

Alisema kutokana na tukio hilo walimkimbiza zahanati ya kijiji, lakini walipofika waliambiwa wampeleke Hospitali ya Sokoine iliyoko Manispaa ya Lindi kwa matibabu zaidi.

Alisema baada ya kufikishwa hospitalini hapo, alipatiwa matibabu kwa siku moja na siku iliyofuata alifariki dunia, maelezo aliyopewa na madaktari ni kwamba sumu hiyo ilikuwa imesambaa mwilini.

Nipashe lilimtafuta Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Sokoine, Dk. Mohamedi Muhaji kwa njia ya simu ili kuthibitisha tukio hilo, lakini simu yake iliita bila kupokelewa.

Hata hivyo, Mkuu wa Kitengo cha Malalamiko katika hospitali hiyo, Dk. Ally Kihaku, alithibitisha kupokelewa kwa mtoto huyo na kulazwa chumba cha uangalizi maalum (ICU) chini ya usimamizi madaktari maalum na kutaja chanzo cha kifo chake kuwa ni kuchelewa kufikishwa hospitalini mapema.

"Huyu mtoto amechelewshwa kufika hapa kwetu, kwani amefikishwa akiwa tayari sumu imeshaenea mwili mzima na kuharibu mifumo ya upumuaji," alisema Dk. Kihaku.

Dk. Kihaku aliwataka wazazi wote kuwa makini na utunzaji wa vitu vinavyoashiria kusababisha usalama wa watu wakiwamo watoto.

# Taasisi kutoa bil. 20/- mkopo w'biashara wadogo

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya kifedha ya Faidika Microfinance Tanzania imetenga zaidi ya Sh. bilioni 20 kwa ajili ya kukopesha wafanyabiashara wadogo na wa kati kupitia programu yao ya 'MKOPO FASTA'.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Faidika Microfinance Tanzania, Baraka Munisi, alisema kuwa mkopo huo hutolewa kwa muda mfupi na masharti nafuu na kuwaomba wafanyabiashara wachangamikie kukopa.

Alisema kuwa sababu ya Faidika Microfinance kutoa mkopo huo ni kuwainua vipato wafanyabiashara ili kuwawezesha kupata maendeleo kama kaulimbiu yao ya 'Lets Improve Life' (tuboreshe maisha) inavyosema.

"Tunajua changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo wafanyabiashara hao na hivyo kuamua kuleta mpango huo maalum wa kuwasaidia kuzikabili changamoto hizo."

Alifafanua kuwa ili mfanyabiashara aweze kupata mkopo, anahitaji kuwa na leseni ya biashara, namba ya utambulisho wa mlipa kodi (TIN) na cheti kilichohidhinishwa cha ushuru, picha, kitambulisho cha serikali kinachotambulika.

"Miezi kadhaa iliyopita Faidika ilizindua programu ya "LetsGO Digital Mall" ambayo inamwezesha mteja wao kupata huduma bora kwa njia rahisi na haraka zaidi. Kupitia LetsGo Digital Mall, mteja anaweza kujihudumia wenyewe kutoka kiganjani mwa simu yake. Tunaamini njia hii itarahisisha mteja kupata mkopo wa kibiashara kwa urahisi zaidi," alisema Munisi.

Mkuu wa Kitengo cha Mauzo, Masoko na Mifumo wa Faidika Microfinance Tanzania, Asupya Nalingigwa, alisema kuwa wamejipanga kutoa huduma bora zaidi kwa wateja wao na kuwaomba kuanza kuwasilisha maombi.

Nalingigwa alisema kuwa taasisi yao inajivunia kutoa huduma bora za kifedha na jambo zuri zaidi ni kuwa na matawi mengi ya kutoa huduma hiyo hapa nchini.

"Ni fursa kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na wakati kupata mkopo kutoka taasisi yetu, tena wenye mashari nafuu na kwa njia ya haraka zaidi. Tunawakaribisha ili kuweza kuinua biashara zao na vilevile kipato," hapa kwetu mambo yote MKOPO FASTA," alisema Nalingigwa.

Alifafanua kuwa ili kuwafikia wateja wengi, taasisi yao imeanzisha namba maalum na mteja anatakiwa kutuma neno FAIDIKA kwenda namba 15062 kisha kuchagua '1' na kuanza kupata huduma kutoka kwa maofisa wao.

# Wafanyakazi waaswa umoja, mshikamano

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI wa Utawala na Rasilimali Watu, Wizara ya Maliasili na Utalii, Prisca Lwangili, amewaasa wahifadhi wa misitu nchini kujenga umoja, mshikamano na kupendana kazini ili waje kuwa na mwisho uliotukuka.

Lwangili alisema hayo mwishoni mwa wiki kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Francis Michael, wakati wa hafla ya kuwaaga wahifadhi misitu wastaafu 61 wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) katika Jengo la Mkuki, Wilaya ya Temeke, jijini Dar es Salaam.

Lwangili alisema, ni heshima kubwa kuwaaga wenzao ambao wamefikia kikomo cha utumishi wao TFS baada ya kuitumikia kwa miaka mingi huku wakiacha alama ya utumishi uliotukuka unaoifanya TFS kuonekana inavyoonekana.

"Nikiwatazama wastaafu hawa naona bado wana nguvu na afya njema, hawa watu wana ujuzi na wamefanya TFS kwa miaka 11 ya uhai wake na tunaona matokeo mazuri walioacha, naamini kuna kanzi data yao watumieni watu hawa.

"Mimi kabla ya kuwa wizara hii nilikuwa Utumishi, TFS ni moja kati ya wakala zinazofanya vizuri sana, tuna wakala 27 zilizoanzishwa kufanya serikali iongeze mapato, kuna nyingine zinasuasua, lakini TFS mko vizuri sana hii maana yake kila mmoja wenu ameshiriki kuifanya TFS hii, na si Kamishna wa Uhifadhi pekee, hongereni kwa hili," alisema Lwangili.

Alitoa wito kwa wastaafu hao wanaporudi uraiani kuendelea kuwa mabalozi wazuri wa uhifadhi na kushirikiana na jamii huku akiwaasa wahifadhi wanaobaki kutambua kuwa kuanza ajira maana yake kuna hitimisho na kuwataka wajipange.

Aliwaasa watumishi waliopo kazini kufanya kazi kwa umoja, mshikamano na upendo. "Ukimpenda mwenzako huwezi kumpiga majungu, huwezi kumuonea wivu zaidi utajenga ukaribu naye ili kile unachokiona kwake halafu kinakupa wivu ujifunze na wewe kikusaidie, na kila mmoja anapokuwa yuko vizuri kwenye eneo fulani, tunatengeneza taasisi yenye mshikamano na upendo na hivyo manung'uniko yatapungua."

Kwa upande wake, Kamishna wa Uhifadhi TFS, Prof. Dos Santos Silayo, aliwahakikishia wahifadhi wastaafu kuwa TFS itaendelea kushirikiana nao katika masuala mbalimbali pale itakapobidi licha ya kuwa wamemaliza muda wao wa kazi.

"Napenda kuwapongeza kwa utumishi wenu uliotukuka hadi kufikia siku ya leo, nipende kuwahakikishia kuwa sisi mnaotuacha kazini tunaamani, mmetuachia misingi mizuri na tutaendelea kuhakikisha taasisi hii inafikia malengo iliyokusudia," alisema Prof. Silayo.

Mhifadhi misitu mkuu mstaafu Valentino Msusa, aliwataka wahifadhi waliobaki kuzingatia sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya serikali na kumwomba Mungu ili wawe na mwisho mwema.

# Wananchi watakiwa kupuuza upotoshaji chanjo UVIKO-19

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa, amewataka wananchi wa Kijiji cha Boimanda, Kata ya Matola kuacha habari za upotoshaji wa chanjo ya UVIKO-19.

Rai hiyo aliitoa katika ziara yake kijijini hapo na kuwataka wananchi kupuuza habari za mitandao ambazo alisema ni uzushi kwamba chanjo hiyo inaleta madhara kwenye afya na kusababisha kifo na upungufu wa nguvu za kiume.

"Ingekuwa chanjo ya UVIKO ina madhara basi Mheshimiwa Rais angekuwa wa kwanza kupata, kwani ndiye aliyeongoza zoezi la utoaji chanjo.

Mimi mwenyewe nimechanja na mpaka sasa bado nipo vizuri.

Tungetaka kuuliwa tungeweza kuuliwa kwa njia mbalimbali, yapo mambo mengi tunapokea kutoka nje ya nchi.

Na huduma ya chanjo haijaanza leo ni huduma ya siku nyingi. Chanjo ni salama na ni kwa ajili ya uhai wetu," alisisitiza.

Wakizungumza baada ya kupata elimu ya chanjo kutoka kwa Mkuu wa wilaya, baadhi ya wananchi wamesema hawakuwa na elimu sahihi kuhusu chanjo ya UVIKO-19.

"Mwanzoni nilikuwa sielewi, maana walisema chanjo zina madhara na wakati mwingine zinaweza kusababisha kifo, lakini nashukuru leo nimepata elimu na nimechanja. Nawashauri wenzangu ambao bado hawajachanja kuhakikisha wanachanja," alisema Winifrida Mgaya.

Naye Joseph Mligo, alisema anashangazwa na watu wanaoielezea tofauti chanjo ya UVIKO-19, "hii chanjo huku vijijini kwenye jamii zetu inaielezewa tofauti kiasi kwamba tulikua tunaogopa, lakini kupitia ufafanuzi huu wa Mkuu wa wilaya yetu tutachanja ili kujiweka salama," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe, anaendelea na ziara yake ya kutembelea katika kila kijiji kuzungumza na wananchi na kutatua kero mbalimbali.




Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Claudia Kitta, akikata utepe kuzindua duka la Tigo, mjini Masasi, mkoani Mtwara juzi. Wapili kushoto ni Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Pwani na Kaimu Ofisa Mauzo Mkuu, Uthoman Madati. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## SHUWASA yabaini hoteli kujiunganishia maji kinyemela

**Na Mwandishi Wetu,** SHINYANGA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA,) imemkamata mteja wao ambaye ni hoteli moja eneo la majengo mapya, Manispaa ya Shinyanga kwa kujiunganishia maji kinyemela.

Tukio hilo lilitokea jana wakati maofisa wa SHUWASA walipofika eneo hilo na kukuta baadhi ya mabomba yamechepushwa na hayapo kwenye mfumo wa dira za maji (mita).

Kaimu Ofisa Uhusiano na Umma wa SHUWASA, Masaka Kambesha, alisema walimtilia shaka mteja huyo na kuamua kwenda kufanya ukaguzi na kukutana na wizi huo.

Alisema bili za mteja huyo zilizokuwa zinatolewa kwake na shughuli anazofanya za hoteli hazikuwa na uwiano.

"Tupo hapa kwa mteja wetu wa maji, tumeamua kumtembelea ili kujiridhisha kama bili zake za maji zina uhalisia na matumizi yake, lakini tumefika hapa tumebaini anatuibia maji," alisema Kambesha.

"Baadhi ya mabomba yamechepushwa hayapo kwenye mfumo wa dira za maji hivyo wanatumia maji bure," aliongeza.

Aidha, Mwanasheria wa mamlaka hiyo, Happy Richard, alisema mteja huyo amekiuka Sheria ya Majisafi na usafi wa mazingira namba 5 ya mwaka 2019, wanakwenda kumchukulia hatua za kisheria kwa mujibu wa sheria ikiwamo kumtoza faini.

# DC akerwa wazee kukosa huduma hospitali za serikali

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, amekerwa na suala la wazee katika Manispaa ya Shinyanga kukosa huduma za matibabu katika hospitali za serikali.

Mboneko alisema alishatoa maagizo kuwa wazee wapewe kipaumbele kwenye huduma hizo ili kuimarisha afya zao.

Alibainisha hayo mwishoni mwa wiki katika mkutano wa hadhara na wananchi wa Ngokolo, Manispaa ya Shinyanga kwa ajili ya kusikiliza kero zao na kuzitafutia ufumbuzi.

Alisema amesikitishwa kusikia baadhi ya wazee kutopata huduma za matibabu katika hospitali za umma.

Alisisitiza kuwa kuna madirisha ya wazee kwa ajili ya kupata huduma kama ilivyoagizwa na serikali.

"Nilishatoa maagizo kwenye huduma zote za afya kuwa mzee apewe kipaumbele na kupata huduma za matibabu nasikitika kusikia malalamiko ya wazee kukosa huduma hizo, nakuagiza Mganga Mkuu wa Manispaa ya Shinyanga, simamia hili, nisisikie tena wazee kutopata huduma za matibabu," alisema Mboneko.

"Wazee mkifika kwenye huduma za afya na kukosa matibabu hakuna kuondoka hadi upate huduma hiyo, nipigieni simu yangu ipo kwenye madirisha ya wazee kwa kila hospitali, nataka usumbufu huu ufe na sisi ni wazee wa baadaye kwanini tuwanyanyase na wakati wote tunaelekea huko," aliongeza.

Katika hatua nyingine, aliagiza itolewe elimu kwa wazee wote kuwa kwenye huduma za afya mfano zahanati kuna baadhi ya dawa hazipatikani.

Alisema inapotokea hivyo kwenye maeneo hayo, wazee wapewe rufani na kwenda kupata dawa kwenye hospitali kubwa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga, Jomaary Satura, alisema ili kuendelea kuboresha upatikanaji wa huduma za matibabu kwa wazee, wametenga Shilingi milioni tano kwa ajili ya kuwakatia kadi za matibabu bure wazee wote katika manispaa hiyo.

Baadhi ya wazee wakizungumza kwenye mkutano huo wa hadhara, walisema kero inayowasumbua ni ukosefu wa huduma za matibabu.

**HABARI KITAIFA**

# Viwango 200 usimamizi mazingira vyaandaliwa

**Na Joseph Mwendapole**

ZAIDI ya viwango 200 vya usimamizi wa mazingira vimeandaliwa vitakavyotumika kwa ajili ya kutengeneza kanuni za usimamizi salama wa mazingira kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Ofisa Viwango vya Mazingira kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Nasra Yusuf, wakati akizungumza na washiriki pamoja na wananchi waliohudhuria tamasha la vijana na mazingira.

Tamasha hilo lilifanyika wilayani Kibaha, mkoani Pwani kwa ajili ya kuwapa wananchi elimu ya masuala mbalimbali ya mazingira.

Nasra alitaja baadhi ya viwango vilivyokwisha andaliwa na shirika hilo kati ya 200, kuwa vinahusisha viwango vya majitaka, uchafuzi wa hali ya hewa, mitikisiko, kelele, taka ngumu na udhibiti wa mazingira.

Alitaja viwango vingine kuwa ni vya moshi wa magari, mionzi na vingine ambavyo ni vya usimamizi wa mazingira ambavyo vinaandaliwa kwa ajili wa kuwawezesha wananchi mazingira yanakuwa salama.

"Kwa hiyo tupo hapa kwa ajili ya kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira na pia kuwezesha wananchi kutambua viwango ambavyo vitawezesha wananchi kuhakikisha mazingira yanakuwa salama kwa sasa na vizazi vijavyo," alisema Nasra na kuongeza.

"Kwa kufahamu viwango tutajua ni kiwango gani cha uchafuzi ambacho mazingira hayawezi kukihimili na mfano ni kelele ambazo zina athari kubwa kwenye masikio na kwenye afya kwa ujumla," alisema.

Alisema viwango vilivyoandaliwa na shirika hilo vimeweka kiasi cha mitetemo wakati wa asubuhi na jioni na sehemu mbalimbali muhimu.

Alitaja baadhi ya sehemu hizo kuwa ni za hospitali na katika maeneo mengine kwenye mazingira ambayo yanazunguka makazi ya watu.

Alitoa wito kwa wananchi kwenda TBS kwa ajili ya kupata nakala za viwango hivyo na ushauri wa jinsi gani wanaweza kuvifikia.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akimpatia hatimiliki ya kimila chifu wa jamii ya wawindaji ya Wahadzabe, Edward Mkumbo. Wapili kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, Sophia Kizigo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahadzabe wapongezwa utayari kupimiwa maeneo

**Na Munir Shemweta,**
SINGIDA

WAZIRI wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameipongeza jamii ya wawindaji ya Wahadzabe, Wilaya ya Mkalama, mkoani Singida kwa utayari iliyouonyesha wa kutambua na kukubali kupimiwa maeneo yao na kupatiwa hatimiliki za kimila.

Jumla ya hatimiliki za kimila 100 zikiwamo 26 zinazomilikiwa kwa pamoja kati ya mke na mume zimetolewa kwa jamii hiyo ikiwa ni hatua kubwa kutokana na kujishughulisha zaidi na uwindaji, utafutaji matunda, urinaji asali na uchimbaji mizizi.

Dk. Mabula alisema, hatua hiyo inaonyesha nia na dhamira njema waliyonayo ya kutaka kuyalinda maeneo yao wenyewe na kushirikiana na serikali.

"Hakika hizi ni salamu na ujumbe wa Rais Samia Suluhu Hassan kuwa jamii ya wawindaji inaungana naye na mkoa tayari kwenda naye sambamba katika kuletea watu wote maendeleo," alisema Dk. Mabula.

Akizungumza na wananchi wa jamii hiyo katika Kijiji cha Munguli, Kata ya Mwengeza, Wilaya ya Mkalama Juni 11, 2022, alisema ni miongoni mwa jamii ndogo nchini ambayo iko katika hali ya kupoteza ardhi wanayoimiliki kutokana na wengine kuingia na kufanya shughuli zisizoendana na tamaduni zao jambo alilolieleza linahatarisha ustawi na maisha na desturi za Wahadzabe.

"Katika miaka ya hivi karibuni jamii hii imekuwa ikikabiliwa na tishio la kutoweka na kupoteza uhalisia wa maisha yao baada ya jamii nyingine kuingia katika maeneo ya mapori ya asili yanayotumiwa na Wahadzabe kwa ajili ya kufanya shughuli za ufugaji, ukulima na hata upasuaji wa mbao jambo alilolieleza limekuwa tishio kwa kiasi kikubwa kwenye jamii hii," alisema Dk. Mabula.

Alitoa mfano wa matishio kwa jamii hiyo kuwa ni pamoja na kupotea kwa makazi ya asili yanayojengwa kwa nyasi kavu chini ya matawi ya miti, wanyama kutoweka, mizizi na matunda kupotea kutokana na mabadiliko ya tabianchi na shughuli nyingine ambazo hazilindi uoto wa asili wa mapori hayo.

Hata hivyo, alisema kwa kutambua athari iliyopo mbele ya jamii hiyo, serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikitafuta njia bora ya kulinda jamii hiyo pamoja na nyingine zinazofanana ili kuhakikisha inajenga usawa kwa watumiaji wote wa rasilimali za ardhi nchini.

Katika kuleta usawa, alisema serikali imeendelea na programu mbalimbali kuhakikisha kila kipande cha ardhi kinapimwa kwa lengo la kuruhusu usawa na ustawi sio wa binadamu pekee bali wa viumbe vyote hai nchini.

Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, Sophia Kizigo alisema, jamii ya Wahadzabe katika eneo hilo la Kijiji cha Munguli, Kata ya Mwengeza, inakabiliwa na changamoto ya mgogoro wa mpaka unaosababisha maeneo wanayotegemea kwa shughuli zao kuharibiwa.

"Changamoto kubwa ya hapa, jamii ya Wahadzabe vyakula wanatoa porini, wanakula asali na nyama za kuwinda na misitu ikiharibiwa au maeneo wanayotegemea kupata vyakula yanapoharibiwa ni changamoto kubwa, hata hivyo, niwapongeze kwa uvumilivu wao," alisema Kizigo.

Bosco Samwel, Diwani wa Kata ya Mwengeza, alimweleza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Mabula, eneo hilo kwa muda mrefu limekuwa na changamoto ya migogoro ya mpaka na wananchi wanaoishi wilaya za jirani za Karatu Arusha na Mbulu mkoa wa Manyara.

Hata hivyo, alisema kwa sasa changamoto zinaelekea kumalizika kutokana na juhudi za Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, Sophia Kizigo, kutafuta ufumbuzi wa migogoro hiyo.

# Waanzishiwa miradi kuepushwa maambukizi VVU

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

WASICHANA balehe na wanawake vijana 975 wenye umri kati ya miaka 10 hadi 24 katika wilaya za Ulanga na Malinyi, mkoani hapa waliokuwa katika hatari ya kuambukizwa na Virusi vya Ukimwi (VVU), wameokolewa baada ya kuanzishiwa miradi ya kujipatia kipato na kujikwamua kiuchumi.

Makundi hayo yamenufaika na mpango huo kupitia Mradi wa Timiza Malengo unaofadhiliwa na Global Fund, Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi (TACAIDS), Shirika la AMREF Health Africa pamoja na Asasi ya Vijana Tanzania (TAYOA).

Ofisa Mradi wa mradi wa Timiza Malengo, katika Wilaya ya Ulanga na Malinyi, kutoka TAYOA, Ekinala Chepe, alisema makundi hayo yameinuka kiuchumi kwa kujenga nyumba za kuishi na wengine kuendelea kufanya miradi mikubwa ya ufugaji na kuwa na ofisi za ushonaji wa nguo.

Alisema mradi huo ulianza mwaka 2019 na sasa upo katika awamu ya tatu ulitambua makundi hayo kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF) katika wilaya hizo na kuanza kutoa mafunzo maalumu ikiwamo elimu ya afya kwa ujumla na jinsi ya kujikinga na VVU.

Mafunzo mengine ni pamoja na elimu ya ujasiriamali, jinsi ya kubuni miradi, jinsi ya kuweka kumbukumbu, namna ya kukabiliana na changamoto za biashara na jinsi ya kupata mikopo katika taasisi za fedha. Alisema baada ya mafunzo hayo walengwa wanabuni miradi wanayotaka kuifanya kwa ajili ya kujiongezea kipato na kupewa mitaji ya kufanya miradi hiyo kuanzia wastani wa Sh. 250,000 hadi 400,000 kulingana na miradi waliyobuni.

Naye Mratibu wa mradi wa Timiza Malengo, Wilaya ya Malinyi, Dk. Zarhia Mngwaya, alisema pamoja na makundi hayo kuibuka na mpango biashara ambao unapitishwa na ngazi ya kijiji na halmashauri, wanafanya kazi ya kufuatilia kwa karibu na wamebaini wengi wanafanya vizuri na kuongeza kipato katika familia na kaya zao na kuleta mabadiliko makubwa. Alisema walengwa hao pia walipatiwa elimu ya upimaji wa VVU, uzazi wa mpango na ukatili wa kijinsia, malezi, makuzi na lishe ambayo imesaidia vijana hao kujielewa.

Dk. Zarhia alisema mradi huo umekuja kutokana na utafiti kuonyesha kuwa wasichana balehe na wanawake vijana walio kati ya miaka 10-24, wako kwenye hatari zaidi ya maambukizi ya VVU na moja ya sababu ni hali duni ya maisha na kukosa kipato. Kwa upande wake, Mratibu wa TASAF Wilaya ya Malinyi, Sylivia Lussumo, alisema miradi hiyo iliyobuliwa na makundi hayo imesaidia kuleta mabadiliko kwa kuwa wasingeipata wangejiingiza kwenye vitendo viovu.

Mratibu wa TASAF Wilaya ya Ulanga, Engilbert Kanyakanya, alisema mradi huo umewezesha kujenga nyumba zao na kubadilisha maisha ikiwamo kusomesha familia ambazo zilishindwa kutokana na hali duni kimaisha.

# Kibaha hatarini kuwa jangwa ukataji miti

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

TAASISI zinazojishughulisha na masuala ya mazingira zimetakiwa kutoa elimu kabla bidhaa hazijaingizwa sokoni ili kudhibiti uharibifu wa mazingira.

Hayo yameelezwa juzi mjini hapa na Kaimu Meneja Msaidizi Rasilimali za Misitu Kanda ya Mashariki, Suleiman Burenga, aliyemwakilisha Kamanda wa Kanda ya Mashariki, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Caroline Malundo, wakati akifunga Tamasha la Mazingira na Vijana.

Burenga aliieleza taasisi hiyo kubadili mtazamo wake wa kushughulika na matamasha pekee na badala yake waandae utaratibu wa kufika maeneo yanapotoka bidhaa kabla ya kufika sokoni.

Alisema umaskini kwenye jamii utaongezeka endapo mazingira hayatatunzwa.

Pia, aliwataka wafanyabiashara kuzingatia ubora wa vifungashio wanavyotumia kufunga bidhaa zao kabla ya kuzifikisha sokoni.

Akizungumza katika tamasha hilo, Mkurugenzi Eustard Rwegoshora wa taasisi hiyo, iliyoandaa tamasha hilo alisema suala la mazingira bado ni mtambuka kwa kuwa wananchi hawajalipa umuhimu.

Rwegoshora alisema jamii inaliona suala la mazingira ni la serikali na zaidi kwa Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) na Baraza la Taifa la Uhifadhi wa Mazingira (NEMC).

"Sio wananchi tu hata baadhi ya Taasisi za serikali bado hazitoi kipaumbele kuhusu mazingira, sisi taasisi yetu inaendelea kuhamasisha utunzaji wa mazingira kwa kutumia nishati mbadala," alisema.

Katika taarifa ya matumizi ya mkaa ya mwaka 2019, Jiji la Dar es Salam linatumia mkaa asilimia 70 ya unaozalishwa nchini, huku Mkoa wa Pwani ukiwa hatarini kuwa jangwa kutokana na kuhudumia Jiji la Dar es Salam katika upatikanaji wa mkaa.



Mhandisi Mshauri wa Kampuni ya Yooshin Engineering Corporation, Moon, akiwaonyesha wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu mpango kazi unaoendelea wa ujenzi wa barabara ya Lusitu - Mawengi (km 50), kwa kiwango cha zege, mkoani Njombe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kamati yashauri vipaumbele ujenzi barabara

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu imeishauri Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi katika ujenzi wa kushirikisha wadau kutoa vipaumbele kwa miradi ya barabara za kiuchumi kwa taifa na ile ya kimkakati ili kufanikisha malengo makuu ya serikali.

Hayo yamesemwa mkoani Njombe na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Selemani Kakoso wakati kamati hiyo ilipotembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa barabara ya Itoni - Ludewa - Manda (km 211.4), sehemu ya Lusitu - Mawengi (km 50), inayojengwa kwa kiwango cha zege na kuridhishwa na hatua zilizofikiwa za ujenzi huo.

"Kamati inaangalia miradi ya kimkakati hivyo wizara katika mipango yenu hakikisheni mnazingatia barabara zitakazokuza uchumi wa taifa na kurudisha gharama kwa haraka," alisema.

Kakoso alisema kuwa ukamilikaji wa barabara hiyo utaenda sambamba na ongezeko la mizigo katika bandari nchini kwa kuwa katika Mkoa wa Njombe ndipo kwenye uzalishaji mwingi wa mazao ya misitu, makaa ya mawe ya Mchuchuma na madini ya chuma cha Liganga na kutaongeza zaidi mapato kwa serikali.

"Mkoa wa Njombe ni tajiri sana kwani una rasilimali kubwa ambazo zinaweza zikatengeneza pato kubwa la taifa na GDP ya kwetu kupanda kwa kiwango kikubwa," alifafanua.

Kamati hiyo pia imempongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kutoa fedha za ujenzi wa miundombinu ya barabara na madaraja kwa wakati na kufungua uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na kuchochea biashara kati ya mikoa kwa mikoa na nchi kwa nchi.

"Tumeelezwa kuwa tayari mkandarasi wa sehemu ya kwanza ya barabara hii kuanzia Itoni - Lusitu (km 50), ameshakabidhiwa eneo kwa ajili ya kuanza ujenzi, hii ina maana kubwa kuwa serikali ipo kazini na inaendelea kuifungua barabara hii," alisema Kakoso.

Vilevile, kamati imeishauri serikali kutafuta fedha kwa ajili ya kuunganisha mkoa wa Njombe na Morogoro kwa barabara za kiwango cha lami kuanzia Kibena - Lupembe - Madeke - Mlimba - Ifakara - Mikumi kwa kuwa ni ya kiuchumi.

Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, aliishukuru kamati hiyo kwa kukagua na kujionea kazi zinavyoendelea za uwekaji zege katika barabara hiyo ambayo ujenzi wake unatarajiwa kukamilika Agosti, mwaka huu.

Kasekenya ameieleza kamati hiyo kuwa serikali iko mbioni kuanza kujenga upya barabara ya Njombe hadi Songea ambayo imekuwa finyu na ilijengwa toka miaka 1980 na tayari Benki ya Dunia imetoa fedha kwa ajili ya uboreshaji.

Awali, akitoa taarifa ya mradi, Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), mkoa wa Njombe, Ruth Shalua, alisema kuwa mpaka sasa ujenzi umefikia asilimia 88 na kilometa 47.3 zimekamilika kwa kiwango cha zege na kazi zinaendelea vizuri, uhakika mradi utakamilika kwa muda uliopangwa na viwango vya ubora.

Nao wabunge kutoka Jimbo la Njombe Mjini, Deo Mwanyika na Mbunge wa Jimbo la Ludewa, Joseph Kamonga, waliishukuru serikali kwa kuendelea kufungua mkoa huo kwa barabara zenye viwango na kuahidi kuendelea kuisimamia miradi yote inayoendelea kwa karibu.

Takribani magari 10,000 yanatarajiwa kupita kwa siku katika barabara ya Itoni - Ludewa - Manda (km 211.4) itakapokamilika kujengwa na kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji na kupunguza muda na gharama za usafiri.

# Wanafunzi HKMU waomba waongezewe mikopo

**Na Joseph Mwendapole**

WANAFUNZI wa fani ya udaktari katika Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (HKMU), wameiomba serikali iwaongezee mikopo wanafunzi wa udaktari na uuguzi na kutoa ruzuku kwa vyuo vya afya ili viweze kudahili wengi zaidi wa fani hiyo.

Ombi hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Rais wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo hicho, Nimrodi Matungwa, wakati akizungumza kwenye hafla ya kufunga kongamano la sita la kisayansi la siku mbili lililofanyika chuoni hapo, jijini Dar es Salaam.

Alisema ingawa serikali imeonyesha kuwajali, lakini kuna kazi kubwa ya kufanya ili kuwawekea mazingira mazuri wanafunzi wa fani ya uuguzi na udaktari kwa kuwa hali ya sasa hairidhishi. "Kwanza tunampongeza sana Rais Samia Suluhusu Hassan kwa mambo mazuri anayoendelea kuyafanya kwenye sekta ya afya ila tunaiomba serikali iangalie uwezekano wa kuvipa ruzuku vyuo vya afya vya binafsi ili viweze kudahili wanafunzi wengi wa fani hii," alisema Nimrodi. Alisema iwapo serikali itawekeza zaidi kwenye fani hiyo na kuwapa mikopo wanafunzi wengi wa fani ya udaktari na uuguzi watapatikana wataalamu wengi wa fani hiyo ambao wanahitajika kwenye maeneo mbalimbali nchini kusaidia kutoa huduma za afya.

"Hali ya mikopo hairidhishi na takwimu zipo ukiangalia hata hapa kwetu wanaopata mikopo kwa ajili ya ada na fedha za kujikimu ni ndogo sana hivyo tunaomba sio tu kwa vyuo binafsi hata vya serikali wapewe hela ya kutosha ya ada na fedha za kujikimu," alisema.

"Kozi zetu ni za muda mrefu sana mfano udaktari ni miaka mitano sasa mtu wa kozi hii akiwa hana mazingira mazuri hasa ya kifedha unamweka kwenye mazingira magumu ya kumaliza masomo yake," alisema Nimrodi ambaye anasoma udaktari mwaka wa tano.

Waziri wa mikopo wa chuo hicho, Elizabeth Mbwambo, alisema ni asilimia ndogo sana ya wanafunzi wa fani ya uuguzi na udaktari wanapata mikopo hali ambayo inawafanya waishi kwenye mazingira magumu.

Alisema fani ya udaktari na uuguzi zinahitaji vifaa maalum vya kuwawezesha kusoma kwa vitendo na serikali inapaswa kuwasaidia kupata vifaa vyote vinavyohitajika kwenye masomo yao kwa kuongeza kiwango cha mikopo na idadi ya wanafunzi wanaopata.

"Ada zetu ni kubwa sasa sio wote wanatoka familia zenye uwezo kuna wakati mwanafunzi anafika mwaka wa pili au watatu anapata changamoto ya kuendelea na masomo kutokana na kushindwa kulipa, wakati mwingine analazimika kuahirisha mwaka wake wa masomo kwa kukosa ada," alisema Elizabeth ambaye anasoma mwaka wa pili uuguzi.

Naye Emilia Kitambala, aliomba serikali iongeze fungu linalotolewa kwa ajili ya utafiti ili kuwahamasisha watafiti vijana kubobea kwenye fani hiyo na hatimaye kuja na majibu ya changamoto nyingi zilizoko nchini.

"Serikali iwape kipaumbele kwenye fungu la utafiti na utafiti ufanyike kuanzia wanafunzi wa shahada ya kwanza ya udaktari utasaidia sana kutoa ushauri wenye manufaa makubwa sana kwa serikali na tunaomba pia iongeze fedha kwenye masomo ya vitendo," alisema Emilia ambaye ni mwanafunzi wa mwaka wa tano udaktari.

Nipashe
Spoti





RONALDO

# WA5 WALIOFUNGA HAT-TRICK NYINGI ZAIDI TIMU YA TAIFA

**LONDON,** England

KUFUNGA mabao matatu 'hat-trick' kwa nchi yako mbele ya maelfu ya mashabiki na mamilioni wanaotazama nyumbani, kunapaswa kuwa moja ya uzoefu wa kuridhisha zaidi kwa mchezaji wa mpira wa miguu.

Ingawa ni soka la klabu ambalo tunapata kulitazama hilo mara kwa mara, soka la kimataifa linakuja na hisia zake za kipekee. Kufunga mabao kwa nchi yako na kuwafanya wenzako wajivunie lazima iwe ndoto kwa wachezaji wengi.

Baadhi ya wafungaji bora wa muda wote wameacha alama isiyosahaulika kwenye anga ya kimataifa.

Sasa hapa tuwatazame wachezaji watano waliofunga hat-trick nyingi zaidi kwa timu zao za taifa katika soka la kimataifa kwa wanaume...

**#5. Lionel Messi (Argentina) – Hat-trick 8**

Lionel Messi ndiye mwanasoka bora zaidi wa wakati wote. Ameweka rekodi ya kushinda Ballons d'Or mara saba katika maisha yake ya kifahari na pia ni mmoja wa wafungaji bora zaidi wa wakati wote. Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 34, aliifungia Argentina mabao matano katika mechi ya kimataifa ya kirafiki dhidi ya Estonia, Juni 5, mwaka huu.

Messi amefunga hat-trick nane kwa timu yake ya taifa. Kwa mabao yake matano dhidi ya Estonia, Messi sasa amekuwa mfungaji bora wa nne katika soka la kimataifa la wanaume, akimpita Ferenc Puskas. Gwiji huyo wa Argentina sasa ana mabao 86 kwa jina lake katika mechi 162 za kimataifa.

**#4. Ali Daei (Iran) - Hat-trick 8**

Ali Daei alikuwa ndiye mchezaji aliyefunga mabao mengi zaidi katika soka la kimataifa la wanaume hadi Cristiano Ronaldo alipompita mwaka 2021. Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Iran alikuwa mshambuliaji hodari na anayetegemewa na anayetajwa sana kuwa mmoja wa wanasoka bora kutoka bara la Asia wa wakati wote.

Katika kilele cha uwezo wake, Daei alichezea timu kama Bayern Munich na Hertha Berlin, ingawa hakufurahia mafanikio mengi huko. Daei amefunga hat-trick nane kwa timu yake ya taifa. Hat-trick yake ya mwisho ilikuwa katika ushindi wa mabao 7-0 wa Iran dhidi ya Laos, Novemba mwaka 2004.

**#3. Ali Mabkhout (Falme za Kiarabu) - Hat-trick 9**

Mchezaji wa kimataifa wa Falme za Kiarabu (UAE), Ali Mabkhout amefunga hat-trick tisa katika maisha yake ya soka na ni mmoja wa washambuliaji bora kuwahi kutokea kutoka barani Asia. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 kwa sasa, anachezea klabu ya Al Jazira ya Ligi ya UAE.

Mchezaji huyo ndiye mfungaji bora wa sita aliyeifungia timu yake ya taifa mabao mengi akiwa amefunga mabao 80 katika mechi 104 za kimataifa. Katika miaka minne iliyopita, Mabkhout amecheza mechi 34 na UAE na kufunga mabao 36.

**#2. Sven Rydell (Sweden) - Hat-trick 9**

Sven Rydell alikuwa mfungaji bora wa muda wote wa Sweden katika soka la kimataifa kwa kipindi cha miaka 82. Zlatan Ibrahimovic alimtoa kwenye kilele cha orodha mwaka 2014 alipofunga bao lake la 50 la kimataifa.

Rydell aliichezea Sweden mechi 43 za kimataifa. Alitikisa nyavu mara 49 na kufunga hat-trick tisa.

Rydell amefunga mabao manne katika mechi mbili katika maisha yake ya soka. Ya kwanza ilikuja dhidi ya Misri, Juni 29, 1924. Ya pili ilikuwa dhidi ya Norway kwenye Mashindano ya Soka ya Nordic ya 1924-28 mnamo Agosti 23, 1925.

**#1. Cristiano Ronaldo (Ureno) - Hat-trick 10**


Cristiano Ronaldo bila shaka ndiye mfungaji bora zaidi katika historia ya mchezo huo. Gwiji huyo wa Ureno ndiye anayeongoza kwa ufungaji mabao katika soka la kimataifa la wanaume. Amekuwa na mchango mkubwa katika kuifanya Ureno kuwa miongoni mwa vikosi vinavyotawala katika ulimwengu wa soka.

Ronaldo amefunga mabao 117 katika mechi 188 akiwa na Ureno. Alifunga hat-trick katika ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Luxembourg katika mechi ya kufuzu Kombe la Dunia la 2022, Oktoba 2021. Kwa kufanya hivyo, Ronaldo akawa mchezaji wa kwanza kufunga hat-trick 10 kwa timu ya taifa katika soka la kimataifa kwa wanaume.

Ronaldo alikuwa muhimu katika kampeni ya Ureno ya kufuzu Kombe la Dunia. Licha ya kuwa na umri wa miaka 37, mshambulizi huyo wa Manchester United bado anaimarika na anaendelea kuwa mmoja wa washambuliaji bora zaidi kwenye mchezo huo.

## ISIKUPITE

HUKU akiwa amemaliza msimu wa Ligi Kuu England na mabao 17 yaliyotokana na mechi 37 alizocheza, Harry Kane ndiye aliyetoa pasi nyingi za mwisho 'assists' kwenye ligi hiyo msimu wa 2021/22, akifanya hivyo mara 19, akifuatiwa na Trent Alexander-Arnold na Bruno Fernandes wenye 'assists'18 kila mmoja.



NIPASHE JUMATATU JUNI 13, 2022




# KLABU 10 ZENYE THAMANI ZAIDI DUNIANI KWA SASA


REAL MADRID

**NEW YORK,** Marekani

MPIRA wa miguu ndio mchezo unaotazamwa zaidi duniani, kwa hisani yake ni chombo kikubwa cha kutengeneza fedha kwa klabu zote zinazohusika. Kila klabu hujishughulisha na mamilioni kila wiki, lakini ni chache tu ambazo huingiza mapato kwa mabilioni mwaka hadi mwaka.

**Timu hizi zinamiliki wachezaji bora zaidi duniani, miundombinu bora na zina mikataba bora kabisa. Mambo haya, pamoja na uungwaji mkono usiozuilika wa mashabiki, hutoa mataji na mafanikio kwa msingi thabiti na hupandisha thamani ya klabu.**

Kwa kuzingatia hilo, hapa tunaangalia klabu 10 zenye thamani zaidi duniani kwa sasa, 2022. Kumbuka: Hii ni kwa mujibu wa utafiti wa Jarida la Forbes. Twende sasa...

### #10. Tottenham Hotspur- Euro Bililioni 2.2

Tottenham Hotspur inaweza kuwa haijashinda kombe kwa takriban miaka 15, lakini klabu hiyo ya Kaskazini mwa Jiji la London, ni moja ya klabu kubwa barani Ulaya kwa sasa.

Spurs msimu huu imemaliza msimu kwa kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, huku kocha Antonio Conte akiunda kikosi cha kuvutia. Klabu hii ina uwanja wa hali ya juu, baadhi ya wachezaji bora katika soka la dunia na kocha wa kiwango cha juu kabisa.

Hivyo, haishangazi kuona wanathaminiwa kwa euro bilioni 2.2 na wanaweza pia kuanza kushinda mataji hivi karibuni.

### #9. Juventus- Euro Bilioni 2.3

Juventus ni wafalme wa Italia na kutawala kwao Serie A katika nyakati za kisasa ni ushahidi tosha.

'Kibibi Kizee' hicho cha Turin kilikuwa kimeshinda taji hilo mara tisa mfululizo, kabla ya kipindi hicho kukatizwa na Inter Milan msimu wa 2020-2021, kutokana na mkakati wa uhamisho wa klabu. Ingawa wamecheza chini ya kiwango chao katika misimu miwili iliyopita, klabu hiyo inapitia hatua ya kujijenga upya.

Bila kujali, Juventus, ambayo thamani yake ni euro bilioni 2.3, itarejea kwa nguvu zaidi msimu ujao huku kocha Massimiliano Allegri akiwa tayari kurudisha kikosi hicho kileleni mwa soka la Italia.

### #8. Chelsea- Euro Bilioni 2.9

Hivi majuzi Chelsea ilipata umiliki mpya huku muungano unaoongozwa na Todd Boehley ukinunua klabu hiyo kwa kitita cha pauni bilioni 4.25. Ingawa kiasi hicho kinaripotiwa pia kujumuisha mkopo wa pauni bilioni 1.6 wa mmiliki wa zamani, unaiweka kwenye nafasi kubwa klabu hiyo.

Roman Abramovich alihakikisha 'The Blues' hao kuwa juu katika ubora wa soka barani Ulaya katika miongo miwili iliyopita kupitia nguvu zake za matumizi zisizo na kikomo. Wamiliki wapya watataka kuendeleza falsafa hii, ingawa huenda wasichukue mikakati sawa ya uhamisho.

Chelsea imekuwa moja ya klabu zinazopambwa zaidi katika soka la Uingereza kwa miaka 20 iliyopita, na thamani yao kwa sasa ni euro bilioni 2.9.

### #7. Paris Saint-Germain- Euro Bilioni 3

Paris Saint-Germain ina moja ya wamiliki tajiri zaidi katika soka duniani na wametawala Ligi ya Ufaransa kwa muongo mmoja uliopita kwa sababu hiyo hiyo.

Klabu hiyo ya Ligue 1 inasifika kwa kununua wachezaji mashuhuri zaidi sokoni, kama inavyothibitishwa na usajili wa Lionel Messi msimu uliopita wa joto. Juu ya hilo, pia wameweza kumbakisha Kylian Mbappe, na hivyo kuthibitisha uwezo wao wa kifedha.

PSG wanaweza kuwa hawajashinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini wanapendelea sana kufanya hivyo wakiwa na utajiri walionao sasa. Thamani ya klabu hiyo ya euro bilioni 3 inaweza pia kuongezeka mara tu watakapopata kombe hilo kubwa zaidi barani Ulaya kwa ngazi ya klabu.

### #6. Manchester City- Euro Bilioni 4

Manchester City wana nguvu kubwa na wamethibitisha hivyo kwa kushinda mataji manne ya Ligi Kuu England katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Kiwango bora cha kocha, Pep Guardiola kimeifanya kuwa moja ya timu bora zaidi barani Ulaya katika muongo mmoja uliopita, shukrani kwa nguvu zao za matumizi na ukuzaji wa wachezaji. Taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya limewakwepa katika kipindi hiki, lakini hawako mbali sana kulitwaa.

Timu hiyo inazalisha vipaji vya hali ya juu katika ngazi ya vijana wakati Uwanja wa Etihad ni mojawapo ya viwanja bora katika biashara. Pia wamemsajili Erling Haaland, ambaye si tu mchezaji mchanga, lakini ni nguzo kubwa ya badaye.

Thamani ya klabu ya euro bilioni nne inaweza kupanda ikiwa itaendelea kushinda mataji na kusajili wachezaji wa aina kama hiyo katika miaka ijayo.

### #5. FC Bayern Munich- Euro Bililioni 4.1

Kama Manchester City, Bayern Munich wametawala ligi yao ya nyumbani nchini Ujerumani bila kuchoka.

Lakini tofauti na mabingwa wa England, miamba hao wa dimba la Allianz Arena hawatumii fedha nyingi kwenye usajili. Wanawinda wachezaji bora kutoka kwa wapinzani wao kwa usajili wa fedha ya kawaida mara kwa mara. Hata hivyo, huwa wanaleta makocha bora zaidi ili kunoa vipaji vyao vya vijana na vilevile kukiweka kikosi chao cha wakubwa kilicho na nyota wengi kucheza katika kiwango cha juu.

Mafanikio yao kwenye hatua ya Ulaya pia yamethibitishwa vema, na sasa wana thamani ya euro bilioni 4.1.

### #4. Liverpool- Euro Bilioni 4.2

Liverpool ndio timu iliyocheza mechi nyingi zaidi barani Ulaya msimu huu. Walishinda Kombe la FA na Kombe la Carabao.

Katika harakati hizo, pia walifanikiwa kumaliza nafasi ya pili kwenye ligi kabla ya kufungwa na Real Madrid kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. Katika kipindi cha miaka saba iliyopita, Jurgen Klopp ameunda kikosi chenye uwezo wa kuleta changamoto katika nyanja zote. 'Wekundu' hao pia wako katika harakati za kujenga uwanja mpya.

Kwa thamani ya euro bilioni 4.2, Liverpool inakuwa katika nafasi ya nne kwenye klabu zenye thamani zaidi duniani, lakini wanaweza kuwa juu zaidi katika orodha hiyo katika miaka michache ijayo.

### #3. Manchester United- Euro Bilioni 4.3

Manchester United hawajashinda taji la Ligi Kuu tangu mwaka 2013 na hawajashinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu 2008. Hata hivyo, hilo halijaathiri hali yao ya kifedha kwani bado wanaingiza mapato makubwa.

Jezi ya vinara hao wa Old Trafford ni mojawapo ya vyanzo vya mapato kama klabu nyingine yoyote maarufu. Aidha, wameendelea kufanikiwa kusajili wachezaji bora duniani kama Cristiano Ronaldo. Na sasa ina thamani ya euro bilioni 4.3.

### #2. Barcelona - Euro Bilioni 4.7

Barcelona walikuwa na msimu wao wenye misukosuko zaidi msimu huu, huku timu hiyo ikifuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya katika wiki chache za mwisho za msimu.

Hata hivyo, baada ya kuwapoteza nyota wengi msimu uliopita wa majira ya joto, akiwamo Lionel Messi, kocha mpya na nyota wa zamani wa Barcelona, Xavi Hernandez tangu wakati huo amekuza vipaji vya vijana kwa nguvu. Zaidi ya hayo, amerudisha mtindo wao wa kuvutia wa kucheza huku akiingia gharama kidogo sana katika mchakato huo.

Hali ya kifedha ya klabu hiyo ni mbaya sana kwa sasa, lakini kuna uhakika mambo yatabadilika baada ya kuwauza nyota wengine msimu huu wa majira ya joto. Pia walitia saini mkataba wa mamilioni ya pauni na Spotify mwaka huu na mambo yanaelekea vizuri kwa klabu hiyo ya Blaugrana, ambayo thamani yake ni euro bilioni 4.7.

### #1. Real Madrid- Euro Bilioni 4.8

Real Madrid ndiyo timu iliyofanikiwa zaidi barani Ulaya na imeweza kuongeza rekodi ya ushindi wa taji la 14 la Ligi ya Mabingwa Ulaya hivi karibuni.

'Los Blancos' hao wamekuwa wakishinda mataji makubwa zaidi kwa muda mrefu. Pia wamekuwa wahafidhina wa kifedha katika misimu ya hivi karibuni, na uwanja wao uliotengenezwa upya pia umefanikiwa. Kwa hiyo, ingawa Kylian Mbappe hatajiunga nao, bado wana uwezo wa kusajili wachezaji bora zaidi kwenye dunia hii.

Kama moja ya timu zinazoshabikiwa zaidi katika soka la dunia, Real Madrid ina thamani ya euro bilioni 4.8.

## Nukuu

"Kuolewa na mchezaji wa soka si jambo rahisi. Naweza kukuambia kesi za wanawake ambao wameolewa na wachezaji muhimu sana wa soka na wanakuambia kwamba wachezaji wanaamini kuwa wao ni Mungu. Wanasema kwamba mahali ambapo Piqué na Shakira walipatana vizuri ni kitandani tu," **Mfanyabiashara Carmen Lomana, ambaye ana uhusiano wa karibu na wanandoa waliotangaza kutengana, Gerard Piqué na Shakira.**



"Hilo haliko nje ya swali. Najisikia vizuri sana Leicester, nilikaribishwa kwa mikono miwili tangu siku ya kwanza. Ninajitoa kwa kila kitu kwa ajili ya klabu hadi siku ya mwisho. Lakini bila shaka unapaswa kusikiliza fursa nyingine, unapaswa kuangalia kazi yako, na wakati mwingine unapaswa kufanya uchaguzi. Labda moja itakuja kwa njia yangu," **Kiungo wa Leicester City, Youri Tielemans akizungumzia kuhusu kutakiwa na Arsenal.**




"Nadhani ni bora kwa Bayern kuwekeza fedha wanazoweza kupata nikiuzwa kuliko kuniweka hadi mwisho wa mkataba, sitaki kulazimisha chochote, hiyo si maana. Natafuta suluhisho bora. Nataka imalizike: hisia lazima zipoe. Nataka kuzungumza kwa utulivu, si kupitia vyombo vya habari. Najua kwamba mzozo unazua vichwa vingi vya habari. Lakini FC Bayern na mimi si maadui, " **mshambuliaji wa Bayern, Robert Lewandowski anayetaka kutimkia Barca**






Straika wa Yanga, Fiston Mayele, ni mmoja wa wachezaji wawili wanaoongoza kwa mabao Ligi Kuu Bara, akicheka na nyavu mara 14, sawa na George Mpole wa Geita Gold FC. **PICHA: MAKTABA**

# REKODI ZA KUSHANGAZA LIGI KUU TANZANIA BARA

**Na Adam Fungamwango**

ZIMEBAKI raundi nne tu kabla ya Ligi Kuu Tanzania Bara kumalizika, huku dalili zote zikionyesha Yanga inakwenda kutwaa ubingwa kwa mara ya kwanza baada ya misimu minne.

**Kwa sasa ligi imesimama kutokana na Kalenda ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Duniani (FIFA), na kwa upande wa Afrika kulikuwa na mechi za kusaka tiketi ya kufuzu michuano ya AFCON, itakayofanyika mwakani nchini Ivory Coast, timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars ikicheza mechi mbili, dhidi ya Niger na Algeria.**

Ligi hiyo inarejea rasmi leo ambapo kuna mechi mbili, Mtibwa Sugar ikiwa nyumbani Uwanja wa Manungu Complex ikiikaribisha Ruvu Shooting, huku Geita Gold ikiwa kwenye Uwanja wa Nyamkumbu, Geita kucheza dhidi ya Dodoma Jiji.

Wakati ligi ikirejea makala haya yanakuletea takwimu na rekodi za timu zote hadi kufikia raundi ya 26, shuka nayo...

### #1. Yanga yaongoza kwa 'clean sheets'

Mpaka sasa Yanga ndiyo timu iliyocheza mechi nyingi bila kuruhusu bao, ikiwa imefanya hivyo mara 19.

Timu hiyo inayoongoza ligi kwa pointi 64, imecheza mechi 26, kati ya hizo imepata 'clean sheets' 19, ikifuatiwa na Simba ambayo imecheza mechi 25 na imefanikiwa kupata 'clean sheets' 14.

Polisi Tanzania inashika nafasi ya tatu ikiwa nazo 12, na timu za Mbeya City, Coastal Union na Kagera Sugar zote zimecheza mechi 11 kila moja, bila wavu wake kuguswa.

Timu ambazo zimepata 'clean sheets' chache kwenye Ligi Kuu mpaka sasa ni Namungo FC na Ruvu Shooting ambazo zimepata sita tu.

### #2. Ruvu Shooting beki inavuja

Ruvu Shooting ambayo inashika nafasi ya 13 kwenye Ligi Kuu, ndiyo timu inayoongoza kwa kuruhusu mabao mengi mpaka sasa. Imeruhusu wavu wake kutikiswa mara 34, ikifuatiwa na Dodoma Jiji ambayo yenyewe imeruhusu mara 32.

Timu zilizoshika nafasi ya tatu kwa kuruhusu mabao mengi kwenye vyavu zake mpaka sasa ni Prisons iliyo kwenye nafasi ya 14 na Mbeya Kwanza inayoburuza mkia, ambazo zote zimeruhusu mabao 31 kila moja. Yanga ndiyo timu iliyoruhu mabao machache zaidi mpaka sasa, ikiwa imeruhusu mabao saba tu.

### #3. Kagera Sugar straika butu

Pamoja na kwamba inashika nafasi ya nane kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa, kwa pointi zake 33, Kagera Sugar ndiyo timu iliyofunga mabao machache zaidi hadi kufikia raundi ya 26.

Imepachika mabao 18 tu mpaka sasa, ikizidiwa hata na timu inayoshika mkia, Mbeya Kwanza ambayo ina mabao 20. Hii inaonyesha kuwa inaongoza kwa kuwa na safu butu ya ushambuliaji msimu huu.

Timu hiyo inafuatiwa na Prisons iliyofunga mabao 19, Mtibwa Sugar, Coastal Union na Mbeya Kwanza zenyewe zimefunga mabao 20 kila mmoja zikiwa kwenye nafasi ya tatu. Timu iliyofunga mabao mengi zaidi mpaka sasa ni Yanga ambayo ina 42, kwa maana kuwa ndiyo timu yenye safu wembe ya ushambuliaji.

### #4. Polisi, Biashara, wazee wa sare

Timu za Polisi Tanzania na Biashara United zinaongoza mpaka sasa kwa kutoa sare nyingi zaidi kuliko zingine kwenye Ligi Kuu. Kila moja imepata sare 12.

Hata hivyo, timu hizo zinatofautiana sana kwenye msimamo wa Ligi Kuu, kwani pamoja na kwamba zote zinafanana kwa sare, lakini Polisi Tanzania ipo kwenye nafasi ya saba kwa pointi zake 33, huku Biashara United ikiwa ya 15 kwa pointi 24. Yanga, Azam, Coastal Union, Prisons na Dodoma Jiji zimepata sare chache zaidi mpaka sasa, kila mmoja akiwa nazo saba tu.

### #5. Prisons ni vipigo tu

Maafande wa Prisons wao wanaongoza kwa kupoteza mechi nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu mpaka sasa. Timu hiyo inayoshika nafasi ya 14 imekumbana na vipigo mara 13, ikifuatiwa na ndugu zao Mbeya Kwanza wanaoburuza mkia ambao wamepoteza mechi 12 mpaka sasa. Yanga ndiyo timu pekee ambayo mpaka sasa haijapoteza mechi yoyote kwenye Ligi Kuu hadi kufikia raundi ya 26.


### #6. Biashara United kushinda mtihani

Biashara iliyo kwenye nafasi ya 15 kwenye msimamo wa ligi, ndiyo timu iliyoshinda mechi chache zaidi mpaka sasa. Imeshinda mechi nne tu, ikifuatiwa na Mbeya City iliyoshinda mechi tano. Yanga ndiyo timu iliyoshinda mechi nyingi zaidi 19, ikifuatiwa na Simba mechi 14.

### #7. Mechi moja mabao kibao

Mechi kati ya Biashara United na Kagera Sugar, iliyochezwa Januari 15, mwaka huu, na kumalizika kwa sare ya mabao 3-3 , ndiyo iliyozalisha mabao mengi zaidi kwa mchezo mmoja mpaka sasa kwenye Ligi Kuu, yakifunga mabao sita.

## JE, WAJUA?



KATIKA karne hii ya 21, Iker Casillas ndiye kipa anayeshikilia rekodi ya kucheza mechi nyingi za kimataifa bila kuruhusu bao 'clean sheets', akifanya kwenye mechi 102, anafutiwa na Gianluigi Buffon (72 ), Hugo Lloris (62), David Ospina (61) na Petr Cech (56).



# Shirika World Vision latoa msaada vifaa tiba

**Na Renatha Msungu,** BAHI

KATIKA kukabiliana na vifo vya wajawazito na watoto wilayani Bahi, Shirika la World Vision Tanzania kwa ufadhili wa Serikali ya Ireland, limetoa msaada wa vifaa tiba vya zaidi ya Sh. milioni 80 ili kusaidia kuondokana na tatizo hilo.

Akipokea vifaa hivyo mwishoni mwa wiki, Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Dk. David Mfinanga, alisema kuanzia Januari hadi Mei mwaka huu, vifo vya watoto vilivyosababishwa na tatizo la upumuaji na wengine kuzaliwa njiti ni saba.

Alisema vifaa vilivyotolewa ikiwamo dawa za kuongeza damu kwa wajawazito, mashine ya oksjeni itasaidia kukabiliana na vifo hivyo.

"Vifaa vya 'baby warm' vya kuongeza joto kwa watoto wanaozaliwa njiti pia tumeletewa itasaidia kuokoa maisha ya watoto wanaozaliwa katika hali hiyo kwenye zahanati mbalimbali hapo Bahi," alisema.

Naye Meneja Mradi wa Afya ya Mama na Mtoto unaotekelezwa katika Wilaya ya Bahi na Chemba, mkoani Dodoma, Daud Gambo, alitaja vifaa vingine kuwa ni dawa za kutibu magonjwa ya kuhara kwa watoto na minyoo na vifaa vya kuhifadhia watoto njiti.

Alisema lengo la kutoa vifaa hivyo ni pamoja na kuisaidia serikali kuboresha sekta ya afya nchini, hususani kwa upande wa mama na mtoto.

"Tumetoa vifaa hivi kwa wilaya hizi, tunaamini vitasaidia kupunguza vifo vya mama na mtoto katika maeneo hayo," alisema Gambo.



Mbunge wa Jimbo la Mvumi, Livingstone Lusinde (kulia), akisalimiana na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa mbele ya wanafunzi wa Shule ya Msingi Mvumi, Wilaya ya Chamwino, walipofika bungeni mwisho wa wiki kujifunza shughuli za Bunge. **PICHA: WAZIRI MKUU**

# Serikali yaweka mkakati upatikanaji soko la zabibu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KUTOKANA na tani nyingi za zao la zabibu kuozea shambani kwa kukosa wateja wa uhakika, Wizara ya Kilimo imeweka mikakati itayowezesha kupatikana kwa soko la uhakika.

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, alibainisha hayo jana alipokuwa akifungua kikao cha wadau wa zao la zabibu kwa ajili ya kujadili mwongozo wa uzalishaji, masoko na uchakataji wa zabibu.

Mavunde, alisema zao la zabibu linakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo uhakika wa soko la ndani na nje ya nchi hali inayosababisha wakulima kulalamika kila wakati wa mavuno.

"Tani nyingi za zao hili la zabibu zimekuwa zikiozea shambani hali ambayo imekuwa kero kubwa kwa wakulima kila mwaka kutumia nguvu nyingi, lakini uhakika wa soko hakuna.

"Hapa Dodoma tumekuwa tukitegemea wanunuzi wawili tu na wao wakishindwa kununua, wakulima mazao yao yote yanaozea shambani," alisema Mavunde.

Alisema kutokana na hali hiyo wizara yake imeweka mikakati ya kutafuta masoko ya uhakika ya zao hilo nje ya nchi ili wakulima wanufaike na kilimo.

Alisema tayari wameshafanya mazungumzo na Balozi wa Burundi na Brazil ambao wamekubali kuanza kununua mchuzi wa zabibu (mvinyo ghafi) ambao watakwenda kuuza kwa kutumia chupa zao.

"Nataka Bunge la bajeti likiisha niende mwenyewe Burundi kwani hawa wapo tayari kununua mchuzi wa zabibu na kwenda kuupaki kwa kutumia chupa zao wenyewe, lakini tumepata soko kutoka Brazil hawa wapo hapa nchini tayari tumeshawatembeza kwenye mashamba yetu na wamekubali kufanya biashara na sisi," alisema.

Pia alisema katika mwaka wa fedha unaoanza mwezi Julai, mwaka huu serikali imepanga kujenga maeneo maalum yatakayotumika kuhifadhia mchuzi wa zabibu utakaokosa wateja.

"Duniani ukiacha nchi ya Chile ni Dodoma peke yake mtu anayelima zabibu anaweza kuvuma mara mbili kwa mwaka, nchi za Kusini mwa Ikweta wanavuna zao la zabibu mwezi Februari hadi Aprili na nchi za Kaskazini mwa Ikweta wanavuna kuanzia mwezi Juni hadi Septemba, lakini Tanzania ina sifa za maeneo yote hayo," alisisitiza Mavunde.

Akizungumzia mwongozo huo alisema utasaidia kuwa na sauti moja kwa wakulima hasa katika masuala ya bei ya zao hilo.

"Hivi sasa hakuna sauti moja kila mkulima anafanya kivyake, hivyo mwongozo huu utasaidia kuwa na bei moja, uhakika wa soko, lakini kupata ufumbuzi wa changamoto mabalimbali," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, alisema ni matumaini ya watu wa Dodoma kuwa wizara hiyo itasaidia kukuza kilimo cha zabibu.

# Chuo chasaidia watumishi kufanyakazi kiufanisi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAFUNZO ya muda mfupi yaliyotolewa na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto kwa watumishi, yamechangia ufanisi wa utendaji wa mahakama.

Mhadhiri wa chuo hicho, Dk. Simon Mlundi, alisema jana kwenye maonyesho ya Baraza la Taifa la Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) yanayoendelea jijini hapo.

Dk. Mlundi alisema chuo kimekuwa kikiendesha mafunzo mbalimbali ya muda mfupi yanayolenga kuongeza ufanisi kwenye utendaji kazi wa mahakama.

Alisema chuo kimeanza kutoa mafunzo kwa njia ya mtandao ambayo watumishi wa mahakama wanapata mafunzo wakiwa katika eneo lao la kazi.

"Mfumo huu wa kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa njia ya mtandao yamesaidia chuo kutoa kozi nyingi zaidi ya 80 kwa watumishi wa mahakama na kuwafikia watumishi wengi kwa muda mfupi," alisema.

Pia, mfumo umeongeza ufanisi kwa majaji na mahakimu wa kushughulikia idadi kubwa ya kesi na kupunguza mrundikano wa kesi katika ngazi zote za mahakama nchini.

"Chuo pia kimekuwa kikitoa mafunzo ya muda mrefu ya kozi ya sheria kwa ngazi ya cheti na diploma, kimekuwa kikitoa mafunzo ya awali kwa majaji na mahakimu wapya, madalali nawatoa huduma wa mahakama," alisema.

Alitoa rai kwa wahitimu wa kidato cha nne na sita wenye sifa kujiunga na mafunzo ya uanasheria kwenye chuo hicho kutimiza ndoto zao.



# Udereva bodaboda unavyookoa vijana uhalifu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SEKTA ya usafirishaji kupitia bodaboda, imetajwa kuwa ni mbinu mojawapo inayotumika kupunguza vitendo vya uhalifu jijini hapo kwa kuwa imetoa fursa ya ajira kwa vijana wengi waliokuwa hawana kazi ya kufanya.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa Umoja wa bodaboda jijini hapa, Aliko Fwanda, wakati akipokea mkopo wa pikipiki sita, zenye thamani ya Sh. milioni 19 zilizotolewa na Taasisi ya Tulia Trust kwa wanachama wa umoja huo.

Alisema bodoboda imetoa ajira kwa vijana wengi na kuwasaidia kutumia muda mwingi kutafuta fedha badala ya kujihusisha na vitendo vya uhalifu ambavyo vinahatarisha maisha yao na wengine.

"Tunaishukuru Taasisi ya Tulia Trust kwa mkopo wa bodaboda ambao una riba nafuu...mbali na faida za kiuchumi pia unatuwezesha kuondoa vitendo vya uhalifu Mkoa wa Mbeya kwa kuwa vijana wote hawa endapo wangekuwa hawana pikipiki labda wangeamua kuwa wezi wa kuvunja nyumba za watu," alisema Fwanda.

Fwanda alisema hadi sasa umoja huo katika Jiji la Mbeya umepokea pikipiki za mkopo 178 kutoka Taasisi ya Tulia Trust na wanachama wake wamekuwa mstari wa mbele kurudisha fedha za mkopo kwa wakati kutokana na usimamizi mzuri wa uongozi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Urlich Matei, alikiri kuwa pikipiki zinazotewa na Taasisi ya Tulia Trust husaidia kupunguza vitendo vya uhalifu kwa kuwa imekuwa sehemu halali ya vijana kujipatia kipato.

"Ni kweli bodaboda zimekuwa msaada sana kwa vijana siku hizi hata matukio ya uhalifu yamepungua...hata ile kusikia watu (vijana) wamechomana visu kwa kuwania mali hatusikii kwa sababu wapo 'busy' kufanya shughuli zao kupitia bodaboda, kwa hiyo mimi naishukuru Taasisi hiyo kupitia kwa Spika wa Bunge Dk. Tulia Akson, kwa kuona umuhimu wa kuwawezesha vijana," alisema.

Meneja wa Taasisi ya Tulia Trust, Jacqueline Boaz, alisema mkopo wa bodaboda jijini humo ni endelevu kutokana na mwenendo mzuri wa kurejesha mikopo kutoka kwa wanachama wanaokopeshwa.

"Tumetoa pikipiki sita zenye thamani ya Sh. milioni 12.2 na kila moja thamani yake ni Sh. milioni 3.2, lakini bado nyingine mbili ambazo zitakuja hapo baadaye ili zitimie nane na hizi zote ni kutoka kampuni ya boxer," alisema Boaz.

Nao baadhi ya wanufuaika wa pikipiki hizo waliishukuru taasisi hiyo, wakieleza kuwa mkopo huo utawasaidia kuwakwamua kiuchumi, huku wakiahidi kurejesha mkopo wao kwa wakati.

"Mimi niishukuru Tulia Trust kwa kutupatia mkopo huu, kwani umekuja kwa wakati mwafaka, utanisaidia kuendesha familia yangu na kuniongezea kipato changu cha kila siku," alisema Kevin Sembele.

# Samia awataka wananchi kuendelea kuliombea taifa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewataka wananchi wa Mkoa wa Mbeya, kuendelea kuliombea taifa ili lifanikiwe katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja viongozi kuendelea kusimamia usalama wa raia.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati wa maandamano ya kumpongeza kwa uongozi mzuri na kuwaletea miradi ya maendeleo alipozungumza kwa njia ya simu na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera.

Rais Samia alipiga simu na kutoa salamu kwa wana Mbeya baada ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kuhutubia wananchi katika viwanja vya kumbukumbu ya Sokoine, jijini humo.

"Niwatakieni kila heri kwenye maandamano na mikutano yenu pamoja na kuendelea kuchunga usalama wa wananchi bila kusahau kuliombea taifa letu," alisema Rais Samia.

Hata hivyo, Homera alisema wana Mbeya wanakiri kwa vitendo mambo makubwa aliyofanya Rais nchini kwa kuboresha miundombinu katika sekta ya afya, maji, umeme, elimu na kilimo.

Alitaja baadhi ya miradi ikiwamo, uboreshaji wa miundombinu katika sekta ya afya ambayo mkoa ulipokea Sh. bilioni 22 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Igawilo, jengo la mama na mtoto, upasuaji, chumba cha kutakasa vifaa tiba, jengo la X-ray pamoja na vituo vya afya vinane.

Alisema kuwa serikali imetoa Sh. bilioni 68 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu mkoani humo.

Katibu Mkuu Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Taifa (UVCCM), Kenani Kihongosi, alieleza kufurahishwa na utoaji wa mikopo ya asilimia 10 inayotolewa kwa makundi ya vijana, wanawake na wenye ulemavu.

Alisema hadi sasa Sh. bilioni 2.6 zimetolewa na halmashauri zote za mkoa huo kwa ajili ya kuwezesha makundi hayo kujikwamua kiuchumi kupitia shughuli za uzalishaji mali.

"Vikundi 241 mkoani Mbeya vimenufaika na mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri kupitia mapato yake ya ndani, vikundi vya wanawake 130 vimenufaika, vijana vikundi 90 na wenye ulemavu 21," alisema Kihongosi.

Mwenyekiti wa CCM, Mkoa wa Mbeya Mchungaji Jacob Mwakasole, alisema kipindi cha mwaka mmoja cha uongozi wa Rais Samia umewarejesha wanafunzi 447 ambao walipata ujauzito wakiwa shule na wanaendelea na masomo.

Alisema kwa sasa wanafunzi hao wanaendelea vizuri na masomo yao ili kutimiza ndoto zao ambazo zilikatishwa baada ya kupata ujauzito.




Baadhi ya taasisi zikionyesha ujumbe wao wa kumpongeza Rais wa Tanzania Samia Suluhu Hassan kwa utawala bora na kuwaletea maendeleo juzi, wakati wa maandamano ya kumpongeza yaliyofanyika viwanja vya Sokoine jijini Mbeya.
**PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Sababu kahawa kutozalishwa kwa tija zatajwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKULIMA wa kahawa, wanashindwa kuzalisha kwa tija kutokana na kutopima afya ya udongo kujua ni mbolea gani inafaa, badala yake wanafanya kilimo cha mazoea na wengine kutojua jinsi ya kuzuia magonjwa kwa kutojua staili za kisasa za ukataji.

Kauli hiyo ilitolewa jana msimamizi mkuu wa shamba la kahawa Utengule Coffe, Amani Ngowi, wakati wa siku ya mkulima, kwa wakulima kufika katika shamba hilo kupata elimu ya kujua kanuni bora za kilimo cha kahawa kutoka kwa wataalamu wa kilimo. Ngowi alisema, alibaini wakulima wengi kushindwa kuzalisha kahawa kwa wingi kutokana na kutopima afya ya udongo, kutokujua mbolea gani inahitajika na kufanya kilimo cha mazoea na wengine kutojua jinsi ya kuzuia magonjwa ya kahawa shambani.

"Kuna magonjwa mengi yanatokea kwenye kahawa, lakini wakulima wengi hawafahamu mfano mwaka jana ugonjwa wa hawa wadudu wadogo walitokea lakini wakulima hawakufahamu jinsi ya kukabiliana nao, tunashauri wakulima wapate elimu ya kilimo cha kisasa pia serikali iwasaidie wapate mbegu bora," alisema Ngowi.

Upendo Sailosi mkulima kutoka Utengule -Usongwe alisema kwa sasa wanakabiliwa na tatizo la wadudu kwenye mimea ya kahawa wanaotoboa miti ya kahawa na kuifanya isistawi na kuoza.

Sailosi alisema kuwa siku ya mkulima ni msaada kwao kwa sababu wanakutana na wataalamu na maofisa ugani kupata elimu ya kukabiliana na wadudu na magonjwa mengine pamoja na kuzalisha kwa tija.

Peter Mwashitete, alisema mafunzo hayo yatawasaidia jinsi ya kuotesha mbegu kisasa, namna ya kukata miti ya kahawa pamoja na uchumaji hadi hatua ya kuvundika.

Alisema, Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB), imewasaidia kupata mafunzo na usimamiaji mzuri zao hilo, kwa kuhakikisha ubora na minada inasimamia bei elekezi iliyoko sokoni.

Meneja wa Kanda ya Mbeya Bodi ya Kahawa (TCB), Sijali Boa, alisema lengo la siku ya mkulima ni kuwasogezea karibu wakulima maofisa ugani na wadau wengine wanaohusika kwenye mnyororo wa thamani wa zao hilo ili kupata mbinu za kuzalisha kwa tija. Alisema matarajio yao baada ya mafunzo hayo ni kuona wakulima wanazalisha kwa kuzingatia kanuni za kilimo na kujikwamua kimaisha kupitia kilimo hicho.





Aisha Ali Khatib, mkazi wa Kijiji cha Tondooni, Mkoa wa Kaskazini Pemba, akichota maji katika bomba lililounganishwa na chemchemu wanayoitegemea. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mradi chemchemu wakomboa wananchi kupata majisafi

**Na Rahma Suleiman,** PEMBA

MRADI wa uboreshaji wa chemchemu katika kijiji cha Mkiang'ombe, Pemba umechangia kuimarisha maisha ya wananchi wa kijiji hicho kwa kuwapatia huduma ya majisafi na salama.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya maofisa wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF) kufika kijijini hapo kuangalia maendeleo ya mradi huo, mwenyekiti wa kamati ya miradi ya jamii katika shehia ya Tondooni, Khamis Hamad, alisema kabla ya mradi huo chemchemu hiyo ilikuwa ikivamiwa na maji ya bahari na wananchi kushindwa kupata maji.

Alisema wananchi wa kijiji hicho wanategemea maji hayo kutokana na kutokuwapo kwa mfumo rasmi wa maji au kisima.

"Mabadiliko ya tabianchi yamesababisha chemchemu kuvamiwa na maji ya bahari na kusababisha ukosefu wa huduma ya maji, lakini kuathiri shughuli za kijamii ikiwamo makazi na maeneo ya kilimo," alieleza mwenyekiti huyo.

Alisema mradi wa uhifadhi wa chemchemu hiyo, uliibuliwa na wananchi na kufadhiliwa na TASAF kwa kujengewa ukuta wa kuzuia maji ya bahari kuingia katika eneo hilo na wananchi kupata majisafi na salama kwa uhakika.

"Chemchemu hii ni ya asili na sisi wananchi tunatakiwa tuilinde hivyo tuliamua kuihifadhi ili kupata maji ambayo ni muhimu kwa matumizi yetu kwa kuwa hapa huwezi kuchimba kisima," alisema.

Aliongeza kuwa licha ya TASAF kutoa ruzuku iliyosaidia kuimarisha miundombinu katika eneo hilo, lakini kuna changamoto ya kupotea kwa kiasi kikubwa cha maji hayo kutokana na ukosefu wa tangi la kuhifadhia maji hayo chemchemu inapojaa.

Mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Aisha Ali Khatib, alisema bila ya chemchemu hiyo wangeshindwa kuishi kwa sababu kijijini hapo hakuna huduma ya maji inayopatikana, chemchemu hiyo ndiyo mkombozi wao. Aliipongeza TASAF kwa kuboresha mradi huo kwa sababu wajawazito na watu wazima walishindwa kufika katika eneo hilo kutokana na miundombinu kutokuwa rafiki.

"Tunaishukuru TASAF sasa hivi tunapata maji, miundombinu ya kufika katika chemchemu imeimarishwa maana awali hali ilikuwa mbaya hatuwezi kufika katika eneo hili," alisema.

Aliiomba serikali kusambaza huduma ya maji kijijini hapo kwa sababu wakati wa kiangazi maji hupungua katika chemchemu hiyo.

"Wakati wa kiangazi maji hukauka katika chemchemu hii na hulazimika kulala bila ya kuoga kwa sababu shughuli zetu za kiuchumi zipo kwenye bahari wanawake tunalima mwani na wanaume huvua."

Alisema licha ya kuwa na huduma ya umeme kijijini hapo, wanatumia umeme wa jua kupandisha maji katika makazi yao na waliiomba serikali kuwaondolea usumbufu wa kupandisha maji kwa kichwa toka kwenye chemchemu hiyo iliyoko bondeni.

Pia waliomba kupatiwa boti itakayosaidia kuwafikisha katika kisiwa cha Njau na vingine wanavyotumia kwa ajili ya shughuli za kilimo na kijamii.

Ziara ya maofisa wa TASAF na waandishi wa habari wa vyombo mbalimbali ilikuwa ya kutembelea wanufaika wa mpango wa kunusuru wa kaya maskini kisiwani Pemba kubaini mafanikio na changamoto zinazowakabili katika utekekezaji wa mpango huo.

Kijiji cha mkiang'ombe, kilichoko katika shehia ya Tondooni, Mkoa wa Kaskazini Pemba kina kaya 536 na walengwa wa mradi 251 waliofikiwa na mpango huo unaotekelezwa Tanzania nzima.

# Waziri ahamasisha uchangiaji damu kuokoa maisha

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Nassor Ahammed Mazurui, amesema kila mtu ana wajibu wa kuchangia damu kwa maendeleo ya jamii kutokana na huduma hiyo kuwa na umuhimu kwa maisha ya binadamu.

Akitoa taarifa kuhusu maadhimisho ya Siku ya Uchangiaji Damu Duniani kwa waandishi wa habari, alisema licha ya watu wengi kuhamasika kuchangia damu bado huduma hiyo inahitajika kwa vile inatumika kila siku.

Alisema kuwa damu nyingi inatumika kwa wagonjwa wanaopata ajali, wajawazito na watoto kwa kuokoa maisha yao.

Waziri Mazrui alisema kwa kawaida siku zote damu huwa inamsubiri mgonjwa na mgonjwa anasubiri damu na kwamba kuna changamoto kubwa katika huduma hiyo.

Alisema benki ya damu inafanya kazi kubwa ya kukusanya damu katika maeneo mbalimbali hasa kupitia mabonanza ya michezo na kuwaomba wadau na wafadhili kujitokeza kwa wingi kuchangia katika mabonanza yanayoanzishwa na benki hiyo.

Alisema mahitaji ya damu kwa mwaka Zanzibar ni chupa 16,000 kiwango kinachofikiwa katika ukusanyaji huo lakini mahitaji yamekuwa makubwa kwa wagonjwa wa ajali.

Alisema, Shirika la Afya Duniani (WHO), linataka nchi kama ya Zanzibar kuwa na chupa za damu kulingana na uwiano wa watu wake kwa asilimia moja ni chupa 16,000 kwa mwaka.

Waziri Mazrui alisema katika kufikia malengo ya kukusanya damu lazima vijana na wananchi wote kuwa mstari wa mbele kuchangia.

Alifafanua kuwa hivi sasa Taasisi ya Mpango wa Taifa wa Damu Salama Zanzibar inafanya kazi kubwa kuwaelimisha wananchi uchangiaji huo ili kuona wakati wote inatumika kwa walengwa wote.

Alisema hajawahi kutokea taasisi hiyo kukosa damu wala mgonjwa kutopatiwa damu kwa sababu hana watu wa kuchangia mgonjwa.

Vile vile, Serikali ya Zanzibar kuptia Wizara ya Afya, inafanya kazi kubwa ya kuwahudumia wagonjwa wanohitaji huduma hiyo ili kuokoa maisha ya mgonjwa.

Kadhalika Mpango wa Damu Salama Zanzibar ulianza mwaka 2005, lakini umeleta maendeleo makubwa kwa wananchi tangu kuanzishwa kwake.

Madhimisho ya Siku ya Damu Salama Duniani huadhimishwa ifikapo Juni 14 ya kila mwaka na kaulimbiu ya mwaka huu kuchangia damu ni kitendo cha mshikamano tuokoe maisha.

# Serikali yahitaji taarifa sayansi ya bahari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, imesema Tanzania inahitaji taarifa sahihi za sayansi ya bahari ili kusaidia kupata matumizi sahihi ya rasilimali zilizoko katika eneo hilo.

Waziri wa wizara hiyo, Suleiman Masoud Makame, alisema hayo alipokuwa akifungua mkutano wa wadau wa sayansi kutoka nchi mbalimbali za mtandao wa Afrika pamoja na Ujerumani, mjini hapa.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuainisha vipaumbele na fursa zilizoko katika eneo hilo na kuiwezesha serikali kupanga mipango sahihi ya matumizi ya bahari.

Kadhalika, alisema taarifa sahihi za dhana ya uchumi wa bahari ni muhimu kuleta maendeleo endelevu ya bahari kupitia nyanja mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kimazingira.

Hata hivyo, alisema serikali imeweka umuhimu mkubwa wa matumizi ya bahari kupitia dhana ya uchumi wa buluu kutokana na eneo hilo ni miongoni mwa maeneo muhimu katika kukuza uchumi wa nchi.

Vile vile, alisema Serikali ya Zanzibar inahitaji kuwa na wataalamu wa kutosha katika mazingira ya bahari ili kusaidia kufanya utafiti wa kutosha ambao itasaidia kuleta maendeleo mapana kwa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

"Kupatikana kwa takwimu sahihi za matumizi ya bahari zitasaidia kwa kiasi kikubwa kufikia malengo ya uchumi wa buluu hapa nchini," alisema.

Alitumia fursa hiyo kuzitaka taasisi na wadau mbalimbali wa sayansi kushirikiana pamoja katika kuleta mabadiliko chanya kwenye kufanya utafiti ili kuwa na taarifa sahihi za sayansi ya bahari ili kuleta maendeleo endelevu.

Akizungumza katika mkutano huo Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais anaeshughulikia Muungano na Mazingira, Mary Maganga, alisema kuna baadhi ya maeneo ya bahari bado yahitaji kufanyiwa kazi kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira ya bahari unaendelea kufanyika siku hadi siku.

Hata hivyo, alisisitiza kuacha matumizi mabaya ya bahari ikiwamo uvuvi usiozingatia sheria kwa kuwa unachangia kwa kiasi kikubwa kuharibu mazalia ya samaki pamoja na kuharibu rasilimali nyingine zilizopo baharini ambazo ni muhimu katika kuendeleza uchumi wa bahari.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Aboud Jumbe, alisema kupitia mkutano huo utaleta tija kubwa kwa Zanzibar kufikia malengo ya dhana ya uchumi wa buluu.

Katibu Mkuu Wizara ya Uvuvi na Mifugo kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Rashid Tamatamah, alisema kuna maeneo serikali yametengwa kwa ajili ya kuyahifadhi na kuleta tija kutokana na kuongezeka kwa mazalia ya samaki, ni vyema kuongezwa maeneo mengine ili yaweze kuwanufaisha wananchi wa Tanzania.

Mkutano huo umewashirikisha wanasayansi wa bahari kutoka nchi tisa za mtandao wa Afrika.

# Watakiwa kutumia takwimu hali halisi mabadiliko tabianchi

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WAANDISHI wa habari mkoani hapo wametakiwa kuandika habari kwa kutumia takwimu zinazozungumzia hali halisi kuhusu bahari, maziwa, mito na fukwe ili kujua ukweli wa mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Takwimu (Open Data Day 2022), ambayo hufanyika kila mwaka, Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari wa Kupinga Matumizi ya Dawa za Kulevya na Uhalifu Tanzania (OJADACT), Edwin Soko, alisema suala la kuongezeka kwa joto duniani linaathiri hali ya bahari na maziwa kutokana na shughuli za kibinadamu.

Alisema ili kukabiliana na hali hiyo, waandishi wa habari wanahitaji kupata takwimu sahihi ingawa kwa Tanzania jambo hilo limekuwa gumu kutokana na upatikanaji wake.

"Tukiandika kwa kutumia takwimu tunaweza kupunguza ukataji miti, moshi unaotoka viwandani na hiyo itasaidia kujua maendeleo ya fukwe mbalimbali nchini na tukaleta mjadala wa matumizi ya takwimu kwenye hifadhi za fukwe, hii inaweza kusaidia hali ya mabadiliko ya tabia nchi kuwa vizuri na kuleta matokeo chanya ndani ya jamii," alisema Soko.

Alisema jamii inahitaji kupata jambo lililo sahihi, ipo haja ya taasisi zinazoshughulika na bahari, maziwa kutoa takwimu zilizoko kwa waandishi wa habari ili waweze kuandika habari za mazingira na hali ya tabianchi.

Soko aliomba serikali kutumia njia mbadala kwa wananchi, inapozuia ukataji wa miti kwa ajili ya kuchoma mkaa.

Waandishi wa habari mkoani Mwanza walishukuru OJADACT kwa kushirikiana na wafadhili wa Shirika la Open Knowledge Foundation kwa kuwapa mafunzo ya kuandika kwa kutumia takwimu.




Meneja wa Mradi wa Afya ya Mama na Mtoto, Daud Gambo (kushoto), akimkabidhi Kaimu Mganga wa Hospitali ya Wilaya ya Bahi, Dk. David Mfinanga (kulia), mashine ya kuongezea joto watoto wanaozaliwa njiti (Baby Warmer) katika hafla ya makabidhiano ya vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 80 vilivyotolewa na Shirika la World Vision kupitia serikali ya Ireland. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Mzabuni akwepa kifungo miaka 3

**Na Samson Chacha,** MARA

MZABUNI wa kukusanya mapato katika minada ya Halmashauri ya Serengeti mkoani Mara, Prisca Mwita, amehukumiwa kwenda jela miaka mitatu au kulipa faini Sh. 700,000 kwa kupatikana na hatia ya ubadhirifu wa mali ya umma Sh. 4,687,000.

Alisomewa hukumu hiyo Juni 8, mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Wilaya ya Mugumu Serengeti, Jacob Ndira. Awali, wanasheria wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Wilaya ya Serengeti, William Lyamboko na mwenzake, Marsha Mseja, walidai kuwa mshtakiwa Prisca akiwa mzabuni wa kukusanya mapato, ushuru wa minada katika Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti, alikiuka taratibu za ukusanyaji na kushindwa kuwakilisha fedha benki alizokuwa akikusanya kati ya Januari 2019 na 2021.

Walidai kuwa katika kipindi hicho kati ya Januari 2019/ 2021, mshtakiwa alikusanya Sh. 4,687,000 bila kuwakilisha benki na kushindwa kuzitolea maelezo ya matumizi yake.

Upande wa mashtaka ulileta mashahidi wanne na mshtakiwa alikiri kosa lake.

Alipotakiwa kujitetea, aliiomba mahakama kumsamehe makosa yake na kudai kuwa ana familia inayomtegemea wakiwamo wanafunzi.

Hakimu Ndira alisema kuwa mahakama imeridhika na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka bila ya shaka na inamtia hatiani kwa ubadhirifu wa mali ya umma kwenda jela miaka mitatu au kulipa faini ya Sh. 700,000.

Pia, fedha alizochukua Sh. 4,687,000 kuzilipa ili iwe fundisho kwa watu wengine ambao sio waaminifu

Mshtakiwa alikwepa kifungo hicho kwa kulipa Sh. 700,000 na fedha alizochukua Sh. 4,687,000.

# Wananchi 1,000 kushuhudia filamu ya Royal Tour

**Na Vitus Audax,** MWANZA

FILAMU inayoelezea vivutio vya kitalii hapa nchini ya Royal Tour inatarajiwa kuonyeshwa rasmi mkoani hapo na kushuhudiwa na wananchi 1,000.

Onyesho la filamu hiyo litafanyika katika ukumbi wa Rock City Mall Juni 18.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi ofisini kwake, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, alisema uonyeshwaji wa filamu hiyo utaambatana na uhamasishaji wa kutembelea vivutio vya ndani ya mkoa na nchi kwa ujumla.

"Tutatembelea vivutio vya ndani ya Mwanza ikiwamo hifadhi ya Saanane, Makumbusho ya Bujora, pamoja na vivutio mbalimbali vilivyoko jijini hapo, vilevile tutakuwa na safari ya kutalii katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti iliyoko mkoani Mara na kwa Mwanza ni safari ya muda mfupi zaidi kufika hifadhi hiyo," alisema.

Aidha, aliwataka wakazi wa mkoa huo kujitokeza ili kuitazama filamu hiyo inayoelezea masuala ya utalii ambayo Rais Samia Suluhu Hassan ameshiriki kuicheza.

"Niwaombe sasa wana Mwanza kufika kwa wingi kuitazama royal tour ikiwa ni pamoja na kuwa na utaratibu wa kufika kwenye vituo vya hifadhi vya Mwanza pamoja na Tanzania kwa ujumla ili kudumisha utamaduni wa utalii wa ndani," alisema.

Kwa upande wake, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi ambaye Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Kisiwa cha Saanane, aliwataka wakazi wa mkoa huo kuwa na utamaduni wa kufanya utalii wa ndani.

"Tumeamua kuifanya hii royal tour hapa Mwanza ikiwa ni kuunga mkono juhudi za Rais wetu Samia Suluhu Hassan katika kulitangaza taifa letu, hivyo niwaombeni wana Mwanza kuwa na utamaduni wa kutembelea vivutio vya hapa mkoani na hata taifa kwa ujumla," alisema.

Kwa upande wake Mkuu wa Kanda Bodi ya Utalii Tanzania Kanda ya Ziwa, Gloria Munhambo, aliwahimiza watu kuhudhuria onyesho hilo ili kuitazama filamu hiyo.

"Tunatarajia kuwa na watu zaidi ya 1,000 katika shughuli hiyo itakayofanyika hapa Mwanza, hivyo niwaombe kuhudhuria kwa wingi ili tuitizame wote ikiwa ni matunda ya juhudi za Rais wetu," alisema.

HABARI KIMATAIFA

## Waandamana kutaka sheria kali ya udhibiti wa bunduki

**New York,** MAREKANI

MAELFU ya watu wameandamana nchini Marekani, kushinikiza sheria kali ya umiliki wa bunduki kufuatia matukio mawili ya urushaji risasi na kusababisha watu 21 kuuawa.

Walioshiriki katika maandamano hayo walibeba kauli mbiu inayosema "Nataka uhuru dhidi ya kupigwa risasi".

Rais wa Marekani Joe Biden aliunga mkono maandamano hayo, akitoa wito kwa Bunge la Congress kupitisha sheria ya usalama wa bunduki haraka.

Licha ya hayo uwezekano wa mabadiliko ya kisheria huenda ukakutana na kikwazo kutoka kwa wabunge wa Republican.

Watoto 19 na watu wazima wawili waliuawa katika shambulizi la Mei 24 katika eneo la Robb Elementary huko Uvalde, Texas.

Shambulio hilo na lile lililotokea Buffalo, New York, ambapo watu 10 waliuawa, limesababisha wito mpya wa kuchukua hatua juu ya udhibiti wa bunduki nchini Marekani.

Juzi kikundi cha usalama cha bunduki cha March For Our Lives (MFOL) - kilichoanzishwa na manusura wa shambulio la risasi katika shule ya Parkland 2018 huko Florida, kilisema kulikuwa na maandamano 450 nchini humo, ikiwa ni pamoja na Washington DC, New York, Los Angeles na Chicago. **BBC**

## China yaapa kupigana kuhusu Taiwan

**BEIJING,** China

WAZIRI wa ulinzi wa China Wei Fenghe, ameapa jana kwamba nchi yake itapigana hadi mwisho kuzuia uhuru wa Taiwan.

Tamko hilo linazidi kuchochea mvutano kati yake na Marekani kuhusiana na kisiwa hicho.

Kumekuwapo na vita vya maneno kati ya madola hayo makubwa duniani, kuhusiana na kisiwa hicho kinachojitawala, ambacho China inakichukulia kama sehemu yake inayosubiri kuunganishwa tena.

Uingiliaji wa mara kwa mara wa ndege za China karibu na Taiwan umeongeza joto la kidiplomasia, na juzi wakati wa mkutano wa majadiliano ya ulinzi wa Shangri-La, Waziri wa Ulinzi wa Marekani Lloyd Austin, aliishtumu China kwa kuendesha shughuli za uvurugaji za kijeshi.

Waziri wa Ulinzi Fenghe alijibu katika hotuba kali kwenye tukio hilo hilo, na kusema Beijing itazimika kupigana ikiwa majaribio yatafanywa kuitenganisha Taiwan na China. **DW**

# Filamu yaibua hasira nchi za Kiislamu

**LONDON,** Uingereza

FILAMU iliyotengenezwa Uingereza ambayo inamwelezea binti wa Mtume Muhammad (S.A.W) imepingwa na nchi mbalimbali duniani.

Serikali ya Morocco imepiga marufuku filamu yenye utata nchini Uingereza inayoitwa Lady of Heaven, baada ya kulaaniwa na baraza la kidini la nchi hiyo.

Filamu hiyo inadai kueleza kisa cha Bibi Fatima, bintiye Mtume Muhammad.

Baraza Kuu la Ulamaa lilisema sinema hiyo ilikuwa ya uongo wa wazi wa Uislamu. Kumekuwa na maandamano ya kupinga filamu hiyo nchini Uingereza.

**Nchi za Misri, Pakistan, Iran na Iraq pia zimepiga marufuku na kulaani filamu hiyo.**

Wiki iliyopita, baadhi ya wanaopinga nchini Uingereza waliandamana kwenye maeneo kadhaa huku zaidi ya watu 120,000 wakitia saini zao isionyeshwe kwenye majumba ya sinema nchini humo.

Nchi za Misri, Pakistan, Iran na Iraq pia zimepiga marufuku na kulaani filamu hiyo.

Baraza hilo lilishutumu filamu hiyo kwa kueleza kuna upendeleo wa kuchukiza na kuwashutumu watengenezaji wa filamu hiyo kwa kutafuta umaarufu na kuumiza hisia za Waislamu na kuchochea hisia za kidini.

Mhariri wa Dini wa BBC, Aleem Maqbool, alisema ukosoaji unatokana na jinsi mtayarishaji filamu na kasisi wa Kiislamu wa Shia, Yasser Al-Habib, alivyowaonyesha watu mashuhuri katika Uislamu wa awali wa Kisunni, akimaanisha kwamba kuna ulinganisho kati ya matendo yao na wale wa kundi la Islamic State la nchini Iraq.

Mtayarishaji wa filamu hiyo Malik Shlibak, aliwakosoa wanaotaka filamu hiyo kufungiwa kwenye mitandao yake ya kijamii na kueleza kuwa ni ushabiki na kuwaambia iwapo hawaipendi filamu hiyo wasiitazame, tofauti na kuizuia.**BBC**



Moshi ukitoka katika kiwanda cha kemikali ambacho kimelipuliwa na vikosi vya Russia juzi. **PICHA: AFP**

# Russia yalipua kiwanda cha kemikali, ndani kuna watu 800 wamejihifadhi

**KYEIV,** Ukraine

MASHAMBULIZI ya makombora yaliyofanywa na vikosi vya Russia, yamesababisha kiwanda cha kemikali katika mji wa Severodonetsk nchini Ukraine, kuwaka moto.

Mapigano makali yanaendelea katika mitaa mbalimbali ya mji huo.

Gavana wa eneo hilo, Serhiy Haidai aliiambia TV ya Ukraine, kuwa moto huo ulianza kuwaka juzi baada ya kuvuja tani za mafuta kutoka kwenye kiwanda cha Azot, na kufanya uharibifu mkubwa.

Maofisa wa nchi hiyo walikadiria kuwa kiasi ya raia 800 wamejihifadhi kwenye kiwanda hicho. Severodonetsk, imekuwa kitovu cha juhudi za wanajeshi wa Russia kusonga mbele mashariki mwa Ukraine.

Jaribio la mapema la Russia kuteka miji mikubwa ikiwa ni pamoja na mji mkuu wa Kyiv, lilidorora na sasa inajaribu kuteka maeneo ya Luhansk na Donetsk ambalo ni eneo kubwa la viwanda.

Kunyakua Severodonetsk na mji wake pacha wa Lysychansk, kungeisogeza Russia karibu na lengo lake kwani kungewapa udhibiti wa Luhansk.

Katika taarifa yake, Haidai alikiri sehemu kubwa ya Severodonetsk sasa iko mikononi mwa Russia. Jeshi la Urusi lilisema kuwa maeneo makazi ya watu Severodonetsk yako chini ya udhibiti wake.

### EU YAAHIDI KUJIBU KUJIUNGA KWA UKRAINE

Rais wa Halmashauri Kuu ya Umoja wa Ulaya Ursula, von der Leyen, amesema halmashauri hiyo itatoa ishara ya wazi wiki ijayo kuhusu azma ya Ukraine ya kujiunga na umoja huo.

Kauli hiyo aliitoa wakati wa ziara yake ya kushtukiza nchini humo juzi, alisisitiza mazungumzo aliyofanya na Rais wa nchi hiyo, Volodymyr Zelensky yatawawezesha kukamilisha tathmini yao kufikia mwishoni mwa wiki ijayo.

Hatua hiyo inakuwa ya kwanza kwanza kwa umoja huo kutangaza hadharani kisio la wakati la kujiunga kwa nchi hiyo.

Rais Zelensky ameshinikiza Ukraine kujumuishwa haraka katika Umoja wa Ulaya ili kupunguza hatari ya kijiografia na kisiasa ambayo imedhirishwa na uvamizi wa Russia Februari 24.

Lakini maofisa wakuu na viongozi wa umoja huo, wanatahadharisha kuwa hata kwa hadhi ya ugombea, uanachama wa Umoja wa Ulaya unaweza kuchukua miaka au hata miongo. **DW**

# NBC YATOA MIL. 50/- UJENZI UWANJA WA KISASA SINGIDA

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara Tanzania (NBC), imetoa kiasi cha Sh. milioni 50 kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa uwanja wa kisasa wa soka utakaojengwa eneo la Mtipa nje kidogo ya Manispaa ya Singida.

**Akizungumza wakati wa hafla ya kupokea fedha hizo juzi, Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Binilith Mahenge, aliishukuru benki hiyo kwa kusikia kilio cha muda mrefu cha wadau wa michezo mkoani humo na kukubali kuchangia kiasi hicho cha fedha.**

"Ni faraja kubwa sana kwetu kuona maombi ya wadau wa mkoa, chama na wawakilishi wetu yamewafikia Benki ya NBC na hatimaye hii leo (juzi), wameamua kutupatia kiasi hiki cha fedha hongereni sana NBC, tutahakikisha fedha hizi zinakwenda kufanya kazi iliyokusudiwa na si vinginevyo," alisema Mahenge.

Mahenge alisema kupitia hatua hiyo, mkoa huo utakuwa kwenye wasaa wa kuweza kuendesha matukio ya kimichezo zaidi kupitia viwanja viwili tofauti ukiwamo uwanja wa zamani, hatua ambayo itayotoa fursa kwa wananchi mkoani humo kufaidika zaidi kwa burudani sambamba na kiuchumi kupitia matukio hayo.

"Kujengwa kwa viwanja vingi vya michezo kutafungua fursa kwa wafanyabiashara wenye mahoteli na makundi mengine ya kupata fedha na hata kuufanya mji wa Singida kupanuka," alisema.

Dk. Mahenge alisema kukamilika kwa viwanja hivyo ambavyo vitajengwa eneo hilo la Mtipa na pembeni mwa barabara ya kutoka Singida kwenda Arusha vitapendezesha mji wa Singida na kuwa kimbilio la wageni kwenda kupumzika kutokana na hewa nzuri inayopatika mkoani humo.

Akikabidhi msaada huo kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Kaimu Mkuu wa Idara ya Masoko na Mahusiano, David Raymond, alisema hatua hiyo ni mwendelezo wa utekelezaji wa sera ya benki hiyo ya kurudisha faida wanayoipata kwa jamii ambayo imejikita katika kuangazia maeneo mbalimbali ikiwamo elimu, afya pamoja na maendeleo ya jamii sambamba na suala la michezo.

"Katika kipindi cha mwaka uliopita NBC tumeweza kusaidia zaidi ya shilingi bilioni moja kwa ajili ya miradi mbalimbali ya kijamii na kiasi hicho ni nje ya shilingi bilioni tisa tuliyotoa kwa ajili ya kudhamini Ligi Kuu ya Tanzania Bara kwa kipindi cha misimu mitatu," alisema.

Alisema wanajivunia kushiriki maendeleo ya soka hapa nchini na kwamba wataendelea kutoa michango kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya michezo kama soka, riadha, gofu na mingine mingi na kuwa benki hiyo inaamini michezo ni afya na ajira.

"Nitumie fursa hii pia kuwakaribisha wakazi wa Singida kwenye tukio letu muhimu la Dodoma NBC Marathoni ambalo litafanyika Julai 31, mwaka huu kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma likiwa na lengo la kukusanya fedha kwa ajili ya matibabu ya saratani ya shingo ya kizazi kwa wanawake kwa kushirikiana na Taasisi ya Saratani ya Ocean Road," alisema.




Kaimu Mkuu wa Idara ya Masoko na Uhusiano wa Benki ya NBC, David Raymond (watatu kulia), akimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Binilith Mahenge, mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 50 iliyotolewa na benki hiyo kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa uwanja wa soka utakaojengwa eneo la Mtipa nje kidogo ya Manispaa ya Singida. Katika hafla hiyo ya makabidhiano iliyofanyika mwishoni mwa wiki mkoani humo, ilihudhuriwa pia na Mstahiki Meya wa Manispaa ya Singida, Yagi Kiaratu (kushoto), Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Singida, Alhajj Juma Killimbah (wa pili kushoto), Mkuu wa Wilaya ya Singida, Mhandisi Paskas Mulagiri (wa pili kulia) na Meneja wa Benki ya NBC Singida, Asia Chembaga. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Mdundo 'Brand Lift' yazinduliwa

**Na Mwandishi Wetu**

PROGRAMU inayoongoza kwa upakuaji wa muziki barani Afrika iitwayo 'mdundo' imezindua chapa mpya ya 'Mdundo Brand Lift', ambayo itawawezesha kuendelea kujitangaza zaidi katika tasnia ya muziki.

Huduma hiyo itakuwa inapatikana kwa watangazaji, katika huduma ya Mdundo Lift, ambapo pia itatoa vipimo vinne muhimu vya chapa ambavyo ni uhamasishaji, kuzingatia, kupendekeza na manunuzi kwa jamii, huku ikifikisha taarifa kwa wakati katika tovuti yake.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa chapa hiyo, Mkuu wa Biashara ya Ubia barani Afrika wa Mdundo, Rachel Karanu, alisema uzinduzi wa chapa hiyo umekuja miezi kadhaa baada ya kutangazwa kuwaingiza katika rekodi watumiaji hai milioni 31 Afrika katika robo ya kwanza ya mwaka 2022, ikiwa ni ukuaji wa asilimia 49 ikilinganishwa na robo iliyopita.

Karanu alisema chapa hiyo ni kipimo ambacho kitawawezesha washiriki wake kufanya maamuzi kulingana na ufahamu wa wateja unaotokana na utafiti walioufanya hadi sasa.

Karanu alisema: "Tumewekeza katika sehemu kubwa ya umiliki wa chapa hii, ili kuhakikisha inasaidia watangazaji kupima utendaji kazi kwa kupitia mashindano baina yao, kwamba kuna watumiaji zaidi ya milioni 33 Afrika nzima kwa utoaji huduma zetu kupitia mtandao. Chombo hiki hutoa maarifa kwa wakati mwafaka na kwa wale wanaotaka kujiongezea kipato na uwekezaji".

Aliongeza, mdundo inakuwa kwa kasi zaidi kwa kutoa huduma ya upakuaji wa muziki na kwa urahisi Afrika, pia imekuwa ikiwarahisishia watangazaji na watumiaji wa muziki kupata huduma wanazozitaka kwa muda mwafaka.

# *Coastal Union fiti kwa Yanga ikiingia kambini*

**Cheji Bakari, Tanga na Adam Fungamwango,** DAR

WAKATI Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda akisema kuwa wapo fiti na tayari dhidi ya Yanga kwenye mchezo wa Ligi Kuu Bara utakaopigwa keshokutwa, Jumatano katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, wapinzani wao hao wameingia kambini rasmi kwa ajili ya mtanange huo muhimu kwao.

Yanga itashuka dimbani katika mechi hiyo ikiwa na lengo la kushinda ili kutawazwa rasmi mabingwa ikiwa imebakiza michezo mitatu kabla ya msimu kumalizika, wakati Coastal yenye pointi 34 katika nafasi ya sita ya msimamo wa ligi hiyo, ushindi kwao ukiwasaidia kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kumaliza nne-bora.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki jijini Tanga, Mgunda alisema wachezaji wote katika kikosi hicho wapo vizuri kiafya na wapo tayari kwa ajili ya mchezo huo.

"Nataka nikwambie kuwa wachezaji wangu wote wapo vizuri katika mechi hiyo muhimu, hakuna majeruhi hata mmoja," alisema.

Alisema kuwa kikosi hicho kinaondoka leo Jumatatu kwa ajili ya mchezo huo ambao kwa upande wa Yanga kwao ni muhimu kwa ajili ya kutangaza ubingwa.

Kwa upande wa Yanga, kikosi cha timu hiyo kimeingia kambini jana kujiandaa na mechi hiyo dhidi ya Coastal Union na nyingine zilizosalia.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, amesema wachezaji wote na wale waliokuwa kwenye timu za taifa, walitarajiwa kuingia kambini jana Kigamboni ili kujiandaa kumalizia msimu.

"Tunaingia kambini Jumapili (jana), tunashukuru wachezaji wetu wote ambao walikwenda kuzitumikia klabu zao za taifa ni wazima, hawajapata majeraha, hatujapata taarifa zozote kutoka kwa madaktari kuwa wana matatizo, hilo ni jambo la kushukuru, kwa hiyo wameshaanza safari na wao wakirejea watajiunga moja kwa moja kambini. Tulikuwa na wachezaji waliokwenda kucheza timu za taifa za Mali, Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na Tanzania," alisema Bumbuli.

Alisema licha ya kwamba kambi hiyo ni maandalizi ya mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Coastal Jumatano, lakini itaitumia kwa ajili ya kumalizia msimu kwa mechi zote tano msimu huu zilizosalia.

"Tuna mechi nne za Ligi Kuu na moja ya fainali ya Kombe la FA, kwa hiyo tunawataka wanachama na mashabiki wetu wajitokeze kwa wingi kwa sababu kwetu ni mechi muhimu sana ambazo zitatupa kile tulichokuwa tunahitaji msimu huu," alisema.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### DEMBELE KUTUA CHELSEA

CHELSEA imepata imani kubwa ya kumsajili winga Mfaransa, Ousmane Dembele baada ya klabu yake ya Barcelona kuthibitisha kwamba nyota huyo mwenye umri wa miaka 25, hajasaini mkataba mpya. ***(Sun)***

### XHAKA KUONDOLEWA

KIUNGO wa Uswisi, Granit Xhaka mwenye umri wa miaka 29 anasakwa na Bayer Leverkusen wakati huu ambao Arsenal inakaribia kumnasa kiungo wa Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 25 kutoka Leicester. ***(Mirror)***

### NUNEZ POA LIVERPOOL

LIVERPOOL imefikia makubaliano ya kumnunua mshambuliaji wa Uruguay, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 22 kutoka Benfica na sasa wanaandaa mkataba tu kukamilisha uhamisho huo wenye thamani ya pauni milioni 85. ***(Guardian)***

### MANE ANUKIA BAYERN

UHAMISHO wa Darwin Nunez unamaanisha kuwa mshambuliaji wa Senegal, Sadio Mane mwenye umri wa miaka 30, anakaribia kutimka Liverpool kuhamia Bayern Munich. ***(Telegraph)***

### RICHARLISON ATAKIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur ipo kwenye mazungumzo mazuri ya kumsajili mshambuliaji wa Everton na Brazil, Richarlison mwenye umri wa miaka 25, kwa ada ya pauni milioni 51. ***(UOL Esport)***

### UNITED KUMKOSA NKUNKU

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Ufaransa, Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 24, anatarajia kubaki RB Leipzig na kusaini mkataba mpya licha ya kusakwa na Manchester United na Chelsea. ***(Leipziger Volkszeitung)***

### ASENSIO AWINDWA ARSENAL

ARSENAL ni moja ya klabu kadhaa zinazofuatilia kinachoendelea kwa Marco Asensio pale Real Madrid, huku hatima ya kiungo huyo mshambuliaji wa Hispania mwenye miaka 26 ikitarajiwa kujulikana wiki ijayo. ***(Mail)***

### CHELSEA KWA LEWANDOWSKI

CHELSEA pia wanajiandaa kuingia kwenye mbio za kumwania Robert Lewandowski, lakini hawawezi kupeleka ofa hadi wamuuze mshambuliaji Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 29. ***(Star)***

### POGBA KUREJEA JUVE

KIUNGO wa Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 29, atarejea Juventus kwa mkataba wa miaka minne wenye thamani ya pauni milioni 68 baada ya kuachana na Manchester United. ***(Gazzetta dello Sport)***

### LENO KUUZWA FULHAM

ARSENAL ipo kwenye mchakato wa kumuuza kipa Mjerumani Bernd Leno mwenye umri wa miaka 30, kwenda Fulham. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# UNITED YAJITOSA KUISAKA SAINI YA LEWANDOWSKI

**Mshambulizi huyo amepania kuhamia kule Barca, lakini uhamisho huo utategemea...**

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United itajaribu kumsajili Robert Lewandowski kama usajili wake kule Barcelona utashindikana, kwa mujibu wa The Sun.

Uhamisho wa Lewandowski kutoka Bayern Munich unazidi kupamba vichwa vya habari na yeye mwenyewe ameshabainisha kuwa hana mpango wa kuendelea kucheza hapo msimu ujao.

Kuondoka Bayern na kujiunga na Barcelona siku zote imekuwa nia ya mshambuliaji huyo, lakini mambo mengine yanatakiwa kuwekwa sawa ili jambo hilo litokee.

> **Kama jambo hilo halitakamilika kwa Barcelona, Man United imejitosa kuwania saini ya mchezaji huyo.**

Mshambulizi huyo wa kimataifa wa Poland amepania kuhamia kule Camp Nou, licha ya kuwa amebakisha mwaka mmoja kwenye mkataba wake na Bayern.

Uhamisho wa kwenda Barcelona utategemea na 'Blaugrana' hao kuuza baadhi ya wachezaji wao wanaolipwa zaidi, huku Frenkie de Jong na Ousmane Dembele wakihusishwa na uhamisho wa kwenda kwingine.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, alifunga mabao 50 katika mechi 46 alizoichezea Bayern katika mashindano yote msimu uliopita.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 253,

MECHI KALI
FRANCE
VERSUS
CROATIA
1 | 1.53
X | 4.05
2 | 5.88

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BARCELONA KUMALIZANA NA GAVI



**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona ina uhakika wa kumpa mkataba mpya kinda wao, Gavi ili aendelee kubakia hapo Camp Nou, kwa mujibu wa rais, Joan Laporta.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17, ndiye mwenye umri mdogo zaidi kati ya vipaji kadhaa vya kusisimua vilivyoko chini ya kocha Xavi.

Gavi aliifungia bao Hispania dhidi ya Jamhuri ya Czech wiki iliyopita na kumfanya kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuifungia timu ya taifa sambamba na mchezaji mwenzake wa Barca, Ansu Fati.

Lakini kiungo huyo mkataba wake wa sasa kwa miamba hao wa Katalunya umebakiwa na miezi 12, ikimaanisha kwamba Barca lazima wachukue hatua haraka kuhakikisha anabaki.

Laporta, rais wa klabu, aliwaambia waandishi wa habari: "Tuna matumaini, kwa sababu tunataka Gavi abaki Barcelona.

"Tunafurahia sana kubaki kwake, anatoka katika akademi yetu. Mchezaji na wakala wake, ambaye tunamfahamu, pia wanataka abakie Barcelona. "Tuko karibu sana kufikia makubaliano."

Hata hivyo, Laporta hakuwa na habari njema kama hizo kuhusu mustakabali wa winga aliye nje ya mkataba, Ousmane Dembele - ambaye alisajiliwa kwa rekodi ya klabu kwa euro milioni 105.

"Dembele ana ofa ya kubaki, lakini hatuna habari kama amekubali," alisema na kuongeza, "Hatujapata jibu kutoka kwake."



## *Keane: Conte atajenga kikosi cha mataji Tottenham Spurs*

**LONDON,** England

ANTONIO Conte anaunda kikosi cha Tottenham Hotspur ambacho hatimaye kinaweza kumaliza kusubiri kwa muda mrefu kushinda mataji, kwa mujibu wa mshambuliaji wa zamani wa klabu hiyo, Robbie Keane.

Spurs walifanya mapinduzi makubwa kwa kumteua Conte kama kocha wao mkuu Novemba mwaka jana baada ya kumaliza mapema muda wa Nuno Espirito Santo.

Kikosi hicho cha London Kaskazini kilikuwa nafasi ya nane kwenye Ligi Kuu ya England wakati Conte anachukua usukani, lakini kipindi cha pili kizuri cha kampeni kiliwafanya kumaliza kwenye nne bora.

Kwa hakika, pointi 71 ambazo Tottenham ilizipata katika msimu wa 2021-22, zilifanya jumla ya alama ambazo wamezipata katika misimu mitatu pekee iliyopita ya Ligi Kuu (86 msimu wa 2016-17, 77 msimu wa 2017-18 na 72 msimu wa 2012-13).

Kuiongoza Spurs kurejea Ligi ya Mabingwa Ulaya kulielezewa kuwa "kombe" kwa Conte, lakini mataji yameikosa klabu hiyo tangu kushinda Kombe la EFL mwaka 2008.

Conte tayari ameanza kukiimarisha kikosi kabla ya msimu wa 2022-23, huku winga mzoefu Ivan Perisic - mshindi wa ligi nchini Ujerumani na Italia - akitarajiwa kujiunga kutoka Inter Julai Mosi, mwaka huu.

HABARI MICHEZO

,545,950

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 14/06/22 | 21:00 | Plaza Colonia CD vs CA Boston River | 2.70 | 3.10 | 2.46 |
| 02. 14/06/22 | 21:00 | San Lorenzo vs Arsenal Sarandi | 2.34 | 2.95 | 3.00 |
| 03. 15/06/22 | 01:00 | Patronato Parana vs Aldosivi | 2.31 | 3.10 | 2.91 |
| 04. 15/06/22 | 03:30 | Juventude RS vs Santos | 2.27 | 2.89 | 3.18 |
| 05. 15/06/22 | 20:00 | Barracas Central vs Union Santa Fe | 2.45 | 3.04 | 2.75 |
| 06. 15/06/22 | 22:30 | Atletico Tucuman vs Lanus | 2.43 | 3.14 | 2.70 |
| 07. 15/06/22 | 22:30 | Banfield vs Central Cordoba | 2.21 | 3.04 | 3.14 |
| 08. 16/06/22 | 03:30 | Atletico Pr vs Corinthians | 2.24 | 2.90 | 3.24 |
| 09. 16/06/22 | 03:30 | America Mineiro MG vs Fluminense | 2.35 | 3.10 | 3.00 |
| 10. 16/06/22 | 22:15 | Keflavik IF vs Stjarnan | 2.70 | 3.48 | 2.26 |
| 11. 16/06/22 | 23:15 | Valur vs Breidablik | 2.61 | 3.44 | 2.35 |
| 12. 17/06/22 | 03:30 | CA Platense vs Gimnasia y Esgrima | 2.66 | 3.00 | 2.56 |
| 13. 17/06/22 | 03:30 | Racing Club vs Velez Sarsfield | 2.36 | 3.10 | 3.00 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATATU - 13/06/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4915 | Chungnam Asan vs Daejeon Citizen | 2.80 | 3.05 | 2.41 |
| 13:30 | 1435 | Ansan Greeners vs Bucheon | 3.47 | 3.18 | 2.01 |
| 14:30 | 5643 | Shenzhen vs Meizhou Kejia | 2.17 | 3.08 | 3.18 |
| 15:00 | 5947 | CA Tigre Reserve vs Boca Jrs | 3.40 | 3.45 | 2.02 |
| 16:00 | 1183 | Bugesera FC vs Police FC Rwanda | 3.63 | 2.85 | 2.11 |
| 16:00 | 1575 | Etoile de Lest vs Gorilla FC | 2.75 | 2.85 | 2.60 |
| 16:00 | 2066 | Marines FC Gisenyi vs Rayon Sports FC | 3.77 | 2.94 | 2.03 |
| 16:00 | 4006 | Gicumbi vs Rutsiro FC | 6.09 | 3.88 | 1.47 |
| 16:00 | 4171 | Musanze vs Mukura | 2.91 | 2.86 | 2.46 |
| 16:00 | 5081 | Raufoss IL 2 vs Molde FK 2 | 3.60 | 4.20 | 1.77 |
| 16:00 | 5672 | Espoir FC vs Kiyovu Sports | 5.69 | 3.48 | 1.57 |
| 17:00 | 2923 | Kazakhstan vs Slovakia | 5.24 | 3.47 | 1.69 |
| 18:00 | 1156 | Seinajoen JK vs Inter Turku | 2.66 | 3.15 | 2.46 |
| 18:00 | 1751 | VPS Vaasa vs HJK Helsinki | 5.49 | 3.78 | 1.53 |
| 18:30 | 3099 | HJK Helsinki W vs ONS Oulu W | 1.05 | 11.00 | 26.00 |
| 19:00 | 1180 | Sierra Leone vs Guinea Bissau | 2.06 | 3.14 | 3.74 |
| 19:00 | 1918 | Czech Republic U21 vs Andorra U21 | 1.03 | 9.83 | 34.40 |
| 19:00 | 5681 | MP Mikkeli vs KuPS Kuopio | 10.83 | 5.51 | 1.21 |
| 19:00 | 5801 | Azerbaijan vs Belarus | 2.32 | 2.99 | 3.29 |
| 19:00 | 5993 | Albania vs Estonia | 1.58 | 3.87 | 5.91 |
| 19:30 | 2903 | IFK Mariehamn vs Hifk | 2.18 | 3.14 | 3.09 |
| 20:00 | 1704 | Eskilstuna W vs Orebro W | 1.80 | 3.58 | 3.78 |
| 20:00 | 2577 | IK Oddevold vs FC Trollhattan | 2.01 | 3.34 | 3.29 |
| 20:00 | 4023 | Kjelsaas 2 vs Lokomotiv Oslo FK | 4.02 | 4.02 | 1.66 |
| 20:00 | 4091 | Stabaek Fotball 2 vs Oppsal IF | 2.26 | 4.21 | 2.38 |
| 20:30 | 5685 | Albania U21 vs Kosovo U21 | 1.61 | 3.74 | 4.72 |
| 21:00 | 4175 | CA Fenix vs Albion FC | 1.69 | 3.59 | 4.33 |
| 21:00 | 5087 | Australia vs Peru | 4.42 | 3.39 | 1.73 |
| 21:30 | 4090 | CA Fenix vs CA San Miguel | 2.31 | 2.84 | 3.18 |
| 21:45 | 1061 | France vs Croatia | 1.53 | 4.05 | 5.88 |
| 21:45 | 2333 | England U21 vs Slovenia U21 | 1.25 | 5.31 | 9.04 |
| 21:45 | 2413 | Denmark vs Austria | 1.87 | 3.34 | 4.25 |
| 21:45 | 4891 | Iceland vs Israel | 2.62 | 3.18 | 2.67 |

### JUMANNE - 14/06/2022

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:00 | 1852 | Nacional Asuncion vs Tacuary Asuncion | 1.99 | 3.25 | 3.45 |
| 00:00 | 4498 | Independiente Fbc vs Rubio NU | 1.91 | 3.04 | 4.02 |
| 00:30 | 4380 | Agropecuario vs Guillermo Brown | 1.99 | 3.00 | 3.78 |
| 01:00 | 1529 | Botafogo RJ vs Avai | 1.69 | 3.39 | 4.71 |
| 01:00 | 4526 | Botafogo SP vs Aparecidense GO | 1.97 | 2.99 | 3.87 |
| 01:30 | 2365 | Defensor Sporting vs Nacional (URU) | 3.39 | 3.34 | 1.98 |
| 02:00 | 1810 | Sport Recife vs Gremio | 3.29 | 2.90 | 2.22 |
| 02:00 | 3737 | Volta Redonda RJ vs Remo PA | 2.32 | 3.15 | 2.85 |
| 02:10 | 4988 | San Martin Tucuman vs Brown Adrogue | 1.71 | 3.14 | 5.10 |
| 02:15 | 2183 | Club Guarani vs Libertad Asuncion | 3.39 | 3.44 | 1.95 |
| 03:00 | 3496 | Nicaragua vs Bahamas | 1.08 | 7.88 | 19.71 |
| 03:00 | 4983 | Guatemala vs Dominican Republic | 1.32 | 4.62 | 8.06 |
| 05:00 | 5805 | Honduras vs Canada | 3.73 | 3.34 | 1.88 |
| 21:45 | 1956 | Poland vs Belgium | 3.49 | 3.44 | 2.03 |
| 21:45 | 2288 | Germany vs Italy | 1.80 | 3.55 | 4.27 |
| 21:45 | 2575 | England vs Hungary | 1.33 | 4.81 | 9.24 |
| 21:45 | 2951 | Netherlands vs Wales | 1.34 | 4.95 | 8.08 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MAKOCHA LIGI KUU NAO WAOMBA KAZI SIMBA SC

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imesema kuwa kati ya maombi zaidi ya 100 waliyopokea kutoka kwa makocha wanaotaka kuifundisha timu hiyo, wapo pia baadhi wanaozifundisha timu kadhaa za Ligi Kuu Tanzania Bara inayoelekea ukingoni.

Mwenyekiti wa klabu hiyo, Murtaza Mangungu, amesema kuwa pamoja na kupata CV za makocha kutoka nje ya nchi wanaozifundisha klabu mbalimbali Afrika na Ulaya, lakini pia wapo wa kigeni wanaozifundisha klabu kadhaa za Ligi Kuu hapa nchini ambao nao pia wameomba kazi ya kuifundisha timu hiyo iliyomtimua kocha wake, Mhispania Pablo Franco, hivi karibuni.

"Tumeshapokea wasifu wa makocha wengi, lakini tutafanya uchambuzi ili tumuajiri mmoja, hili si jambo geni kwa klabu kama ya Simba kupata maombi mengi, tunayo zaidi ya 100 sasa, wapo wa nje ya nchi, lakini tuna CV pia za makocha wa ndani, wageni wanaozifundisha klabu za hapa ndani za Ligi Kuu nao wameomba pia. Sasa nani atafanikiwa kuwa kocha hayo si maamuzi ya kwangu, ni maamuzi ya kikao, tutafanya kikao na kufikia uamuzi yupi atatufaa zaidi," alisema Mangungu.

Hii itakuwa ni mara ya kwanza baada ya muda mrefu makocha wanaofundisha Ligi Kuu kuomba kazi Simba, kwani wakati wa mchakato wa kumpata kocha aliyeondoka, klabu ya Simba ilidai hakukuwa na kocha yeyote anayefundisha Ligi Kuu, iwe mgeni au mzawa aliyepeleka wasifu wa kuomba kuifundisha timu hiyo.

Kwa sasa klabu hiyo ipo kwenye mchakato wa kumsaka kocha, ambapo hivi majuzi, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema wanataka kocha huyo mpya angalau ashuhudie mechi nne au tatu za Ligi Kuu ili awaone wachezaji waliopo na kutoa ushauri wake, lakini awe na mchango mkubwa kwenye kusaka baadhi ya wachezaji watakaosajiliwa kwa msimu ujao.

Hata hivyo zipo taarifa pia kuwa huenda kocha wa zamani wa Kaizer Chiefs, Stuart Baxter ndiye akawa Kocha Mkuu wa timu hiyo, baada ya kuonekana kwenye picha kadhaa mitandaoni akifanya mazungumzo na Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Barbara Gonzalez.




Mshambuliaji wa Timu ya Bulls, Ben Mango, akiruka juu kumiliki mpira kwa kichwa dhidi ya mabeki wa timu ya General ya Tegeta, zilipokutana kwenye Mashindano ya Dar Youth Cup yaliyohusisha vijana wenye umri wa chini ya miaka tisa, 11 na 13 kutoka timu mbalimbali lengo likiwa ni kuibua na kuendeleza vipaji vya soka la nchini Tanzania. Mechi hiyo ilipigwa viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# *Aggrey ajifunga tena mwaka Azam FC*

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha wanaimarisha kikosi chao, uongozi wa Klabu ya Azam, umemwongeza mkataba wa mwaka mmoja beki wake, Aggrey Moris.

Aggrey ambaye mkataba wake unafikia ukingoni mwishoni mwa msimu huu, tayari ameongeza mkataba wa mwaka mmoja kuitumikia timu yake kwa msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano mingine iliyopo mbele yao.

Akizungumza na gazeti hili jana, beki huyo alisema bado yuko sana ndani ya kikosi cha Azam FC na msimu ujao ataonekana ndani ya timu hiyo akiipambania kutafuta matokeo mazuri katika michuano iliyopo mbele yao.

Alisema hakuna ukweli wowote yeye kuhusishwa na klabu zingine kwa sababu ameongeza mkataba wa kuitumikia Azam FC baada ya makubaliano ya pande zote mbili kufikia muafaka.


"Tayari nimeongeza mkataba wa mwaka mmoja na nitasalia kuitumikia Azam FC kwa msimu mwingine, kuhakikisha tunafikia malengo yetu ya kutwaa ubingwa na kupata nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa kwa msimu ujao," alisema Aggrey.

"Ligi Kuu tumetwaa ubingwa mara moja, lakini mashindano mengine tumetwaa mara nyingi ni mafanikio, malengo ya Azam ni kutwaa ubingwa wa ligi, hivyo yapo na yanaendelea kupambaniwa na msimu huu hatujayafikia kama ilivyokusudiwa," alisema beki huyo.

# Michezo

Jumatatu Juni 13, 2022

Nipashe

Barca kumalizana na Gavi UKURASA 22

CHUMA HICHO...



Winga wa Simba, Kibu Denis akifunga moja kati ya mabao mawili aliyoifungia timu yake wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Cambiaso, kwenye mechi ya kirafiki ya mazoezi iliyopigwa Uwanja wa Mo Simba Arena, Bunju nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam jana. Mabao ya Cambiaso yote yalifungwa na Simon Msuva. **PICHA: SIMBA**

## Yanga yashinda mbio saini straika wa Kaizer

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Yanga imeripotiwa kuwa mbioni kushinda vita vya kuinasa saini ya mshambuliaji wa Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini, Lazarous Kambole kwa mkataba wa miezi sita wenye kipengele cha nyongeza ya miaka miwili.

Kwa mujibu wa chanzo chetu ndani ya klabu hiyo, Yanga imeipiku Zesco United katika vita vya kuwania saini ya mshambuliaji huyo raia wa Zambia ambaye ameifungia mabao mawili tu katika mechi 24 alizoichezea tangu ajiunge na timu hiyo mwaka 2019.

"Ni kweli ni mmoja wa washambuliaji ambao Yanga wanamhitaji na wapo katika nafasi nzuri ya kumpata kwani Kaizer Chiefs inaonekana kutohitaji huduma yake kwa sasa," kilieleza chanzo chetu.

Licha ya kutokuwa na nyakati nzuri hapo Kaizer Chiefs, Kambole, alikuwa na msimu mzuri wakati akiwa na miamba ya Zambia, Zesco United kabla ya kujiunga na klabu hiyo ya Afrika Kusini.

Kambole, anakumbukwa vema kutokana na rekodi yake ya kufunga hat-trick ya haraka zaidi (ndani ya dakika tano za mchezo) kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika wakati Zesco United ikiibuka na ushindi wa mabao 3-0 ugenini dhidi ya Mbabane Swallows Agosti 18, 2018 nchini Eswatini.

Mshambuliaji huyo alifunga mabao hayo katika dakika ya 38, 40 na 43 akamilisha hat-trick yake.

Yanga ambayo tayari ina tiketi ya kuiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, ipo katika harakati za kukiimarisha kikosi chake kuelekea msimu ujao, licha ya kwamba ligi bado haijamalizika.

# Simba yatangaza jeuri ya usajili

### Beki kisiki wa Chippa United ya Sauzi atajwa, waeleza kukwepa vita vya Al Ahly, Berkane kuwapora...

**Na Saada Akida**

WAKATI Simba ikielezwa kuwa katika mazungumzo na beki wa kati wa Chippa United ya Afrika Kusini na timu ya Taifa ya Burundi, Frederic Nsabiyumva, ili kuja kuimarisha safu ya ulinzi ya kikosi chao, uongozi wa klabu hiyo ya Mtaa wa Msimbazi jijini Dar es Salaam, umesema katu haushindwi kumsajili nyota yeyote wanayemhitaji.

**Simba ipo katika harakati za kuimarisha safu yake ya ulinzi baada ya kudaiwa kuwa mwishoni mwa msimu huu itaachana na beki wake wa kati, Muivory Coast Pascal Wawa, ambaye umri kisoka umeanza kumtupa mkono.**

Hata hivyo, licha ya kuendesha mambo yao kwa siri kubwa ikiogopa kuzidiwa ujanja na wapinzani wao, tayari imeelezwa kuwa Simba imeanza mazungumzo ya kuipata huduma ya beki huyo wa Burundi aliyekuwa hapa nchini na timu yake ya taifa na kuichezea juzi katika mchezo wa kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2023 dhidi ya Cameroon ambao uliopigwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Burundi iliutumia Uwanja wa Benjamin Mkapa kama wake wa nyumbani kutokana na viwanja vya nchini kwao kutokidhi vigezo vya kimataifa.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Klabu ya Simba Salim Abdallah 'Try Again', amesema: "Tumejifunza kuwa na weledi mkubwa kwenye usajili, maana wapinzani wetu, Al Ahly, Orlando, Berkane wanafuatilia kila tunapopiga hodi. Sasa kama tutakuwa tunatembea na kamera kupiga picha na wachezaji tunaowafuatilia, itakuwa shida, wanachama na mashabiki wa Simba tuachieni sisi kazi ya kusajili."

Lakini akizungumza na gazeti hili jana, Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema Rais wa Heshima na Mwekezaji wa klabu hiyo, Dk. Mohammed "Mo" Dewji, ametenga kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya usajili ili kukiimarisha kikosi cha timu hiyo kuelekea msimu ujao wa michuano iliyopo mbele yao hususan Ligi ya Mabingwa Afrika na Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alisema hawashindwi kumsajili mchezaji mzuri na ikitokea hivyo, sababu kubwa ni klabu yake kuhitaji kiasi kikubwa cha fedha ambacho ni tofauti na thamani ya uwezo na kiwango cha mchezaji husika.

"Sisi Simba tunajua tunahitaji nini, mchezaji gani tunahitaji kumsajili, hatutaki kusajili kwa mihemko au kushindana na mtu. Tunafanya usajili kulingana na mahitaji yetu, lakini hatuwezi kusajili hadi hapo tutakapompata kocha mkuu ambaye atakuwa na jukumu hilo.

"Kikubwa tunafanya usajili mkubwa, kama alivyosema rais wa heshima, kuna maboresho makubwa yanakuja katika usajili kwa kuleta watu wenye uwezo na kiwango bora na kuifanya Simba kuwa tishio zaidi msimu ujao hasa katika michuano ya kimataifa," alisema Ahmed.

Alisema kuna wachezaji wa maana ambao wanafanya mazungumzo nao na anasubiriwa kocha mpya ambaye atapewa taarifa za wachezaji wote waliopo na pia kuona kikosi cha timu yake na kupewa majina ya wachezaji ambao wanafanya mazungumzo na Simba.

"Niwahakikishie mashabiki wa Simba kwamba hatufanyi usajili kupitia mitandao ya kijamii, wachezaji ambao watakuja kwa msimu ujao watakuwa tishio na nina imani kuna jitu litakufa," alisema Ahmed.

Alisema hakuna mtu yeyote ambaye alikuwa akimjua Pape Ousame Sakho na Henoc Inonga, lakini wachezaji hao wamesajiliwa na kufanya vizuri zaidi ndani ya kikosi cha Simba na baadhi ya klabu kuhitaji huduma zao.

Wakati huo huo Kikosi cha Simba jana asubuhi kilicheza mechi ya kirafiki ya mazoezi dhidi ya Cambiasso FC, mchezo uliopigwa katika Uwanja wa Mo Simba Arena na wenyeji kushinda 3-1.

Katika mechi hiyo, Simba walianza kwa kasi na kuliandamana lango la Cambiasso ambapo dakika ya pili tu Kibu Denis aliipatia bao la kwanza baada ya kupokea pasi ya kutoka Pape Sakho.

Baada ya bao hilo Simba waliendelea kushambulia lango la wapinzani hao ambapo Kibu tena alitupia bao la pili dakika 36 kwa kisigino akimalizia pasi ya Yusuph Mhillu.

Saimon Msuva aliwafungia Cambiasso bao la kwanza dakika ya 40 baada ya kuwazidi ujanja walinzi wa Simba kabla ya Sadio Kanoute kufunga la tatu na kufanya kwenda mapumziko Wekundu wa Msimbazi wakiwa mbele kwa mabao 3-1.

Kipindi cha pili Kocha Selemani Matola aliwapumzisha Inonga, Pascal Wawa, Kanoute, Gadiel Michael, Kibu na Sakho na kuwaingiza Joash Onyango, Mzamiru Yassin, Kenedy Juma, Mohammed Hussein, Jimmyson Mwanuke na Taddeo Lwangwa, lakini mabadiliko hayo hayakuweza kusaidia kuongeza bao badala yake Msuvu alirudi kambani na kuiandikia Cambiaso bao la pili lililofanya mechi kumalizika kwa matokeo ya mabao 3-2.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042


9 770856 541002 >